Jumatatu Mei 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580591

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Mwinyi** aeleza alivyosafiri chumba kimoja kwenye meli na mbakaji, mporaji

UKURASA 3



**Ujenzi** reli ya kisasa kuwekewa mfumo wa kisasa kudhibiti ajali

UKURASA 3



**Manny Pacquiao ulingoni Agosti**

UKURASA 21

# Ajira kizungumkuti

• **120,000** waomba nafasi 9,675 zilizotangazwa na serikali... *Endelea Uk.2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**MAMIA DAR WAMZIKA MFANYAKAZI WA VODACOM**
VILIO na simanzi vimetawala kuagwa kwa mwili wa Meneja Mauzo wa kampuni ya...

UKURASA WA 4
**MWINYI KUWAADABISHA WAHUSIKA UPOTEVU FEDHA**
RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali...

UKURASA WA 8
**LHRC YAJITOSA SAKATA LA WASICHANA KUTOROSHWA**
KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimefanya ziara ya kuitembelea...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Ripoti ya Hesabu za Serikali na Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali, Ikulu jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## 'Tatoo' zawaponza vijana kupata mafunzo JKT

UKURASA 2



Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago (wa pili kusho-to), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa kampeni ya Mastaboda ji-jini Dodoma inayolenga kuwakopesha vijana bodaboda na pikipiki za miguu mitatu, jijini humo mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi na mwisho kulia ni Mkuu wa Idara ya Kadi NMB, Philbert Casmir, Mkuu wa Idara ya Biashara, Alex Mageni na Mwenyekiti wa Wendesha Bodaboda Dodoma, Kenneth Chimoti. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mtumbwi wazama, sita wa familia 2 wahofiwa kufariki

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO **NURKOVIC WA KAIZER AIPIGIA SALUTI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# 'Tatoo' zawaponza vijana kukosa mafunzo JKT

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya vijana wilayani Kahama, mkoani Shinyanga waliokuwa wanaomba nafasi za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wamekosa sifa baada ya kubainika kuwa na michoro kwenye miili yao (tatoo).

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema amesikitishwa na vitendo vya vijana wasomi kujiingiza kwenye masuala ya 'ulimbukeni' kwa kuiga na kujichora michoro sehemu mbalimbali za miili yao.

Alisema kuwa mtu akijichora mwilini anapoteza sifa ya moja kwa moja ya kujiunga na jeshi lolote hapa nchini na kuwataka vijana wanaotaka kujiunga na jeshi hilo mwakani wahakikishe hawana michoro yoyote katika miili yao.

"Walioomba kujiunga na jeshi hili walikuwa 96, tumechakata kwa kina zaidi na kupata vijana 20 kulingana na uhitaji wa nafasi zilizokuwa zinahitajika, 15 kwa vijana wa kidato cha nne na tano vijana wa elimu ya darasa la saba. Wengi wamekosa sifa kwa sababu mbambali ikiwamo na kujichora mwilini," alisema Macha.

Aliwataka vijana kuacha kuiga vitu na kujikuta wakifanya mambo yasiyofaa ambayo yanawagharimu na kutoa tafsiri mbaya wanapokuwa watu wazima.

Pia, aliwataka wazazi na walezi kuendelea kutoa malezi bora kwa vijana wao ili kuwanusuru na matatizo mbalimbali za maisha.

Aliwaasa waliochaguliwa kujiunga na mafunzo hayo kutotegemea kuajiriwa serikalini badala yake watumie nafasi hiyo kwenda kupata ujuzi watakaofundishwa kwa manufaa yao ya baadaye baada ya kuhitimu mafunzo.

Aliwataka vijana kuzingatia nidhamu na taratibu zote watakazozikuta huko kwa kuwa kumekuwa na vijana wengi wanaopoteza nafasi zao hizo wakiwa kambini kwa utovu wa nidhamu.

Mkazi wa Kata ya Nyahanga, Denis Kasindi, alisema vijana hao wamekosa nafasi kutokana na kukaa mitaani muda mrefu na kuanza kujifunza mambo mabaya kiwamo kujichora miili yao.

Kwa upande wake, Rehema Bajora, mkazi wa Kata ya Nyahanga, alisema ili kuwasaidia vijana wa mtaani ratiba za maombi ya kujiunga na jeshi hilo zitolewe mapema ili kuwasaidia kutojiingiza kwenye makundi mabaya.

# 120,000 wawania ajira 9,600 serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZAIDI ya watu 120,000 wamejitokeza kuwania nafasi 9,675 za ajira zilizotangazwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kada ya afya na elimu.

Hadi jana idadi ya watu walioomba katika kada ya afya walifikia 31,673 kati ya 2,726 wanaohitajika, wakati kada ya elimu walioomba walifikia 89,959 kati ya 6,949 wanaohitajika.

Hata hivyo, Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, ameongeza siku tano zaidi kwa waombaji, kutokana na wengine kushindwa kukamilisha maombi yao.

Mei 9, mwaka huu, Waziri Ummy alitangaza maombi ya ajira za walimu wa shule za msingi, sekondari na watumishi wa kada mbalimbali za afya.

Alisema maombi hayo yataombwa kuanzia Mei 9 hadi Mei 23, mwaka huu kwa njia ya mtandao, kwamba kati ya ajira hizo walimu ni 6,949 na afya ni 2,726.

Waziri Ummy alisema ajira hizo zitajaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliokoma utumishi, kutokana na sababu mbalimbali.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi hiyo, Nteghenjwa Hosseah, ikimnukuu Waziri Ummy ilieleza kuwawali waombaji walitakiwa kutuma maombi yao kuanzia Mei 9, mwaka huu na mwisho ulikuwa Mei 23.

Katika taarifa hiyo, Waziri Ummy alisema hadi Mei 21, mwaka huu saa 5:59 usiku, waombaji wapya waliosajiliwa kwenye mfumo wa maombi ya ajira kwa kada ya afya ni 49,951, ambao maombi yao yamepokelewa kwa ukamilifu ni 31,673.

"Katika maombi ya kada mbalimbali za afya waombaji waliosajiliwa ni 49,951 na ambao maombi yao yamepokelewa kwa ukamilifu ni 31,673 waliobaki hawajakamilisha kujaza taarifa zao kwenye mfumo," alisema Waziri Ummy.

Aidha, alisema kwa upande wa elimu waombaji wapya waliosajiliwa kwenye mfumo ni 20,975 na waliohakiki taarifa zao za awali kwa kada hiyo ni 78,808, jumla ya waombaji waliosajiliwa ni 99,783.

Hata hivyo, alisema kati ya waombaji hao waliosajiliwa, maombi ambayo yamepokelewa kwa ukamilifu ni 89,958 wengine bado hawajakamilisha taarifa zao kwenye mfumo.

"Hawa ambao maombi yao yamepokelewa kwa ukamilifu katika mfumo yaani wamejaza kwa asilimia 100 na kukamilisha maombi yao, lakini wapo ambao hawajakamilisha kwa asilimia 100 wamejisajili kwenye mfumo, tumeongeza siku tano ili nao wakamilishe maombi yao," alisema Waziri Ummy.

Aliwasisitiza waombaji ambao walishindwa kukamilisha taarifa zao kwenye maombi ya ajira kutumia muda huo uliooongezwa kukamilisha kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bunge, jijini Dar es Salaam ambao ni mabalozi wa Usalama Barabarani wakitoa elimu ya usalama barabarani kwa moja ya madereva wakati wa Maadhimisho ya wiki ya Usalama barabarani kimataifa jana, ambapo kwa hapa nchini, Kampuni ya Mafuta ya Puma imeungana na Umoja wa Mataifa pamoja na Shirika la Afya Duniani( WHO) kuadhimisha siku hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtumbwi wazama, sita wa familia mbili wahofiwa kufa

**Na Gideon Mwakanosya,** NYASA

WATU sita wa familia mbili katika Kijiji cha Mipotopoto, mkoani Ruvuma, wanahofiwa kufa maji, baada ya mtumbwi waliokuwa wakisafiria kuzama katika Mto Ruvuma.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji mkoani Ruvuma, Mkaguzi Msaidizi Chesco Mbata, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12 asubuhi katika eneo la Mto Ruvuma.

Aliwataja watu hao ni Yusuph Ummy (28), Fitina Salum (22), Fahim Ummy (2), Tosha Kalomba (30), Emran Chiponda (1), Rambo Mohamed Chiponda (6).

Alisema siku hiyo ya tukio, watu hao wa familia mbili walikuwa wakitokea nyumbani kwao na kwenda katika shughuli zao za kilimo kwa kutumia usafiri wa kienyeji wa mtumbwi maarufu kwa jina la gome, kwamba walipofika katikati ya mto mtumbwi ulizidiwa na kasi ya mawimbi ya maji na kusababisha kupoteza muelekeo na kuzama majini.

Alifafanua zaidi, Kaimu Kamanda Mbata alisema baada ya kupokea taarifa hizo kutoka katika uongozi wa kijiji cha Mitomoni kupitia Jeshi la Polisi Wilayani Nyasa, Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ngazi ya Wilaya na Mkoa walifika eneo la tukio na kuwakuta wananchi wakiendelea kuwatafuta watu hao.

Alisema katika juhudi za uokoaji walifanikiwa kupata mwili wa Emran Chiponda, alikimbizwa katika Kituo cha Afya cha Liparamba ambako baadaye alifariki dunia wakati anaendelea kupatiwa matibabu. Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, alitoa wito kwa wananchi ambao wanazunguka Ziwa Nyasa na mito mikubwa yote iliyopo wilayani humo kuchukua taadhari wanapovuka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema jitihada za uokoaji zinaendelea .

# Mwinyi aeleza alivyosafiri na mhalifu chumba kimoja melini

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesimulia namna alivyopatwa na hofu akiwa safarini kurejea nchini akitokea masomoni jijini London, Uingereza, baada ya kukaa chumba kimoja kwenye meli na mhalifu wa uporaji na ubakaji.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasimulia hayo akisema mwaka 1956 akiwa pamoja na wenzake wawili kutokea Zanzibar, walikutana katika Jiji hilo, kusomea masomo tofauti na walipomaliza walianza safari ya kurudi Tanzania.

Anasema walikuwa wakisoma katika vyuo tofauti, yeye akisomea ualimu huku Dk. Awadhi aliyekuwa akisomea utabibu na Makame akisoma utawala, walikutana katika safari moja ya kurudi nchini baada ya kuchagua kutumia usafiri wa meli.

"Tulikuwa wanafunzi watatu tuliotoka Zanzibar, kila mmoja alisoma taaluma tofauti. Sote watatu tukaamua kutalii; tukachagua kusafiri kwa meli. Tukakatiwa tiketi ya kusafiri kwa meli ya Afrika Kusini iliyokuwa inaitwa Doneta Castle," anasema Mwinyi.

"Wakati huo ndiyo ubaguzi wa rangi unatokota Afrika Kusini. Tukapewa chumba kimoja sote watatu. Kwenye meli yote ile chumba chetu peke yake ndicho kilichokuwa na watu weusi."

Mwinyi anasema wakati meli ikikaribia kung'oa nanga majira ya mchana, ndipo walishuhudia mtu ambaye alikuwa mwenye asili ya Kisomali akiingizwa chumbani kwao akiwa na pingu mkononi.

"Tukajua yule mwenzetu lazima atakuwa mhalifu mkubwa, vinginevyo asingeletwa melini akiwa ametiwa pingu. Mimi na wenzangu Dk. Awadhi na Makame, tukashauriana kwa Kiswahili juu ya mbinu za kusalimika tuwapo na bwana yule.

"Tukakubaliana tujenge urafiki, tukawa tunachangishana fedha kidogo na kumkabidhi kwa ajili ya matumizi yake, ikiwamo kununulia sigara," anasema Mwinyi.

Anabainisha, baada ya urafiki kujengeka akawasimulia uhalifu alioufanya Uingereza, ikiwamo kufanya wizi, unyang'anyi, kupigana na kubaka na kwamba uamuzi wao ulikuwa ndiyo salama yao hadi walipofika Bandari ya Mombasa, Kenya, kisha polisi kumchukua na kuondoka na mhalifu huyo.

Mwinyi anasema wakati meli hiyo ilipotia nanga maeneo kadhaa, ikiwamo Genoa nchi Italia, walitembea katika fukwe huku dada mmoja Muitaliano akimfuata Dk. Awadhi na kumkumbatia.

"Maria Africano. Huyo Maria akaja pamoja rafiki zake wakatualika twende nao mahali ambapo walituambia wana vyumba tunakoweza kwenda kupumzika na kustarehe. Tukajua hawa ni makahaba na tukienda nao yanaweza kutukuta makubwa, pengine kuibiwa na hata kuuawa," anasema Mwinyi.

Anasema baada ya kuondoka eneo hilo na meli ikipita katika mfereji wa Suez Canal, Misri, kulikuwapo joto kali na kuamua kurudi chumbani na alipotokea kaburu na kuanza kufoka na kuwatusi huku akimpiga Dk. Awadhi.

"Akasema anataka kupigana na sisi mmoja baada ya mwingine. Tukaamuuliza kulikoni, akajibu; mmemsukuma mke wangu, akamshika mkono mkewe na kuondoka naye," anasimulia Mwinyi katika kitabu hicho.

Mwinyi anasema: "Usiku baada ya chakula, kulikuwa na muziki ndani ya meli na wao walishiriki, tukamuona yule Kaburu na mkewe. Akatuomba radhi."

## Reli ya kisasa kuwekewa mfumo wa kudhibiti ajali

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limesema katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kutawekwa mfumo wa kisasa ambao utasaidia kuzuia ajali zitakazojitokeza wakati wa uendeshaji wa treni.

Pia, mfumo huo hautamruhusu dereva kuzidi ama kupunguza mwendo uliowekwa.

Meneja Msaidizi wa mradi wa reli ya kisasa, kipande cha Morogoro - Makutopora chenye urefu wa kilometa 422 wa shirika hilo, Mhandisi Christopher Mang'wela, aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza na wahandisi kutoka serikalini na sekta binafsi ambao wametembelea mradi huo ambao ujenzi wake umefikia asilimia 61.

Alisema mradi umefika asilimia 61 na uendeshaji wake utakuwa ni wa kisasa kwa kuweka vifaa maalum vya kumuongoza dereva wa treni ili kuzuia ajali.

Awali, akizungumza kwa niaba ya wahandisi hao, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Mhandisi Patrick Barozi, alisema nia na uwezo kwa Watanzania katika kusimamia miradi mikubwa inayoendelea nchini ameiona licha ya kuwa na usimamizi mdogo kutoka kwa raia wa nje.

Hata hivyo, alisema kupitia vipande vitatu vya utekelezaji wa mradi huo, wahandisi wa nchini wamepata utaalamu wa kutosha na itasaidia serikali katika utekelezaji wa awamu zinazofuata endapo watawezeshwa upatikanaji wa vifaa.

Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mhandisi, Dk. Ramadhan Mlinga, aliwahimiza wahandisi waliopo kwenye mradi huo kufuatilia kwa makini kipindi cha mwisho cha utekelezaji wa mradi huo ili kuboresha utekelezaji wa miradi inayofuata.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

ADAM MATHEW KIJA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA PASSO yenye namba za usajili T 133 CKK chasisi namba KGC100013058 engine namba IKR00019480,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
DAR/KIJ/RB/133007/2021



**KADI YA BAJAJI**

DEOGRATIAS MUMENYA MWIJAGE anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji aina ya TVS BAJAJI yenye namba za usajili MC 288 BQU,yeyote atakayeikokta atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
MBE/MBE/RB/
245023/2021


## Ni wiki ya bajeti kilimo, ardhi na uvuvi bungeni

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

NI wiki ya makadirio ya Wizara tatu zinazogusa maisha ya Watanzania wengi ambazo zitawasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Leo na kesho Wizara ya Kilimo itawasilisha bajeti yake ambayo matarajio ya wengi ni kwa namna imejipanga kuboresha sekta hiyo ambayo ni uti wa mgongo wa nchi na inategemewa na Watanzania zaidi ya asilimia 70 waishio vijijini na mjini wakiwa ni watumiaji wakuu wa chakula kutoka huko.

Aidha, kilio kikubwa cha wakulima ni uongezaji thamani wa mazao yao ili kuondoka na kuuza mazao ghafi na badala yake kuuza bidhaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi. Ladhalika, jinsi ya kuyafikia masoko hayo kwa wakati kabla bidhaa zao hazijaharibika na kuwa na viwanda muhimu vya kuongeza thamani mazao kama nyanya, matunda na mbogamboga ambazo hupatikana kwa msimu mmoja kwa wingi na mengi kuoza kabla ya kufika sokoni.

Jumatano na Alhamis itakuwa ni zamu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi, ambayo inatarajiwa kueleza namna imeshughulikia tatizo sugu ya migogoro ya ardhi, ikiwamo uvamizi wa ardhi, migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa nchini hasa vijiji vilivyosajiliwa ndani ya Hifadhi za Taifa Tanzania.

Wiki hii itafunga dimba kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwasilisha makadirio yake na matarajio makubwa ni namna uchumi wa bahari unaweza kutumika kama chanzo kikuu cha mapato badala ya kutegemea vinywaji.

Akihutubia Bunge, Rais Samia Suluhu Hassan, alirejea kauli ya Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, kuwa mfugaji ana kundi kubwa la mifugo kiasi yeye (mfugaji) hanenepi na mifugo hainenepi.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**SALOME HENRY SANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0683-0084** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KALENGA** mwaka **2015**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**DAR/MSI/RB/220844/2020**



**EMPLOYMENT OPPORTUNITY**

**Tire Sales Manager & Filed Sales Staff with MRF's Tanzania Distributors**

**About MRF:** MRF is India's largest tyre manufacturer and ranked amongst the Top 20 Global Manufacturers with 9 state-of-the-art factories across India. MRF is also India's largest Original Equipment Manufacturer (OEM) tyre supplier with an expansive tyre range from two-wheelers to fighter aircrafts.

**Individuals with Sales & Network Development experience in (any of) Tire, Spare Parts, Accessories, Oil are encouraged to apply.**

**Prerequisites for Sales Manager:**
Minimum 5 years of experience with proven skills to lead a team Field Sales Staff, achieve monthly business plans, growing market share through sales development/ network expansion, ability to make MS Excel & Power Point presentations, are encouraged to apply.

**Prerequisites for Filed Sales person:**
Minimum 2-3 years of field sales and promotional experience is a must.

**Other desired qualifications:**
Valid 2W Driving License.
Good fluency in English will help to participate effectively in training programs.
Should have proven

**Work Station:** In any of major towns in Tanzania.

**Pay Scale:** As per years of experience and agreed between the candidate and the respective distributor management.

**Candidates with above mentioned qualifications are encouraged to apply through mrftzsales@gmail.com on or before 15th June 2021.**

**Disclaimer:**
*This an MRF Initiative to scout for good Tanzanian talents & support Tanzania distributor's business.*
*The CV's or Bio-Data received will be shared with the distributors for their shortlisting of candidates.*
*The call for interview will be from the distributor offices only.*

# Mapendekezo 5 kuboresha biashara nchini

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge la Viwanda na Biashara, imetoa mambo matano muhimu kwa serikali kuzingatia kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa kamati hiyo, David Kihenzile, alisema pamoja na hatua nzuri zinazoendelea kuchukuliwa na serikali, bado kuna malalamiko kutoka kwa wawekezaji kuhusu mazingira rafiki ya kufanyia biashara na uwekezaji nchini.

Alisema baadhi ya wawekezaji wanalalamikia uwapo wa changamoto kama mamlaka nyingi za udhibiti, urasimu katika upatikanaji wa vibali vya uhamiaji na mlolongo wa kupata vibali vya uwekezaji.

"Taarifa ya Benki ya Dunia inaripoti Tanzania kuwa katika nafasi ya 141 kati ya 190 ya nchi yenye mazingira rahisi ya kufanyia biashara nafasi ambayo si nzuri sana," alisema.

Alitaja mambo matano ambayo yakitekelezwa kutakuwa na mabadailiko ni serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria ya uwezeshaji wa Biashara (Business Facilitation Act) ili uwasilishwe bungeni haraka na kusaidia kutatua changamoto hizo.

Jingine ni kuongeza nguvu/kasi katika utekelezaji wa Blueprint ili kuondoa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo wazalishaji na wafanyabishara nchini.

Pia, kuzisisitiza na kuzisimamia sekta zote za serikali kuhakikisha zinatekeleza sehemu yake katika Blueprint.

Kamati hiyo ilishauri kufanyika mapitio ya kodi mbalimbali kwa nia ya kuzipunguza kwa kutazama majirani za kikanda ili kushindana nao katika masoko ya ndani na kikanda.

Jingine ni kutoa elimu kwa wananchi kuhusu blueprint ili kurahisisha utekelezaji wake kwa kuwa kila mtu ana nafasi yake katika kuongeza ufanisi na kasi katika kuleta maendeleo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Kihenzile, ni muhimu kuwapo ufunganishaji sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo pamoja na ujenzi wa viwanda kwa kuanzisha viwanda

vitakavyochakata mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji, na kwa kuzingatia asilimia kubwa ya Watanzania wanajihusisha na shughuli hizo.

Kuhusu bidhaa feki, alisema uwApo wa bidhaa bandia au zisizokidhi viwango sokoni unadhihirisha bado kuna ushirikiano mdogo/hafifu baina ya taasisi za ukaguzi katika vituo vya mipakani pamoja na gharama kubwa inayotozwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kwa mujibu wa Kihenzile, ni muhimu serikali ikaimarisha Shirika la Viwango (TBS) pamoja na Tume ya Ushindani (FCC) kuhakikisha wanatekeleza maju-

# Dk. Mwinyi kuwaadabisha waliohusika upotevu wa fedha

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kuchukua hatua kali kwa wote waliohusika na kasoro zilitolewa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili kasoro hizo zisije kurudiwa tena.

Aliyasema hayo jana baada ya kukabidhiwa Ripoti za Hesabu za Serikali kwa mwaka 2019 -2020, Ikulu Zanzibar, hafla ambayo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alisema fedha nyingi za Serikali zinapotea kwa kiasi kikubwa na iwapo hali hiyo itaendelea maendeleo hayatoweza kupatikana katika kuijenga nchi.

Alisema lengo na madhumuni ya kupokea ripoti hiyo hadharani ni kuhimiza uwajibikaji na utawala bora kwani ni lazima Serikali iwe wazi na kujulikana changamoto ndipo itakapowezekana kukabiliana na matatizo kama hayo.

Aliongeza kwamba katika taasisi za ukusanyaji wa fedha bado kuna upotevu wa udhaifu wa mifumo, hata dhamira ovu ya watendaji katika ukusanyaji wa fedha za Serikali.

Alisisitiza kwamba mbali ya suala la ukusanyaji pia katika taasisi hizo kuna udhaifu wa matumizi hali inayosababisha upotevu mkubwa wa fedha za Serikali. Alisema haiwezekani ionekane kumepokewa tu taarifa hiyo bali ni lazima hatua zinazohitajika zikachukuliwa hasa ikizingatiwa kwamba fedha hizo zinahitajika katika kuimarisha miradi ya maendeleo.

Alisema kuwa ni lazima ripoti hiyo ikafanyiwa kazi ili ripoti ya mwakani kusije kujitokeza kasoro kama hizo.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alieleza kusikitishwa kwake pale watendaji wa Serikali wanaposhindwa kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Serikali na kusema kwamba jambo hilo ni kukengeuka Katiba ya Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alieleza kwamba baada ya kukabidhiwa ripoti hiyo kinachofuata ni kupelekwa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutolewa maoni. Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar Dk. Othman Abbas Ali alisema kuwa amekabidhi ripoti hiyo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Ibara ya 112 pamoja na sheria nyengine zinazompasa kufanya hivyo.

Aliongeza kuwa ukaguzi alioufanya umebaini katika Hesabu za Mfuko Mkuu wa Serikali kuwapo kwa baadhi ya upungufu katika uandaaji na uwasilishwaji wa hesabu jumuishi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020.

# Mamia wamzika mfanyakazi wa Vodacom



Kaburi la aliyekuwa Meneja Mauzo wa kampuni ya simu ya Vodacom, Jimson Kibiki (36), Ununio, Dar es Salaam.

**Na Beatrice Shayo**

VILIO na simanzi vimetawala kuagwa kwa mwili wa Meneja Mauzo wa kampuni ya simu ya mkononi Vodacom, Jimson Kibiki (36), aliyeuawa kwa risasi na watu wanaodaiwa kuwa majambazi, Dar es Salaam.

Mei 20, mwaka huu Kibiki alipigwa risasi na watu hao akiwa anaingia nyumbani kwake baada ya kuchukua fedha benki.

Baada ya kufikishwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) akiwa anapatiwa matibabu alifariki duniani.

Ibada ya kuaga mwili huo ilifanyika jana majira ya saa 7:10 mchana katika Ushirika wa Kanisa la Kiinjili la Lutherani (KKKT), Kunduchi.

Mamia ya watu walijitokeza kuaga mwili huo huku simanzi zikitawala kanisani hapo na makaburini.

Ibada hiyo iliongozwa na Mwinjilisti wa Kanisa hilo, Joseph Giyo, ambaye alisema baada ya kupatiwa taarifa za kuuawa kwa Kibiki ziliwasikitisha.

Alisema marehemu alikuwa mtu mwenye upendo na mwenye kupenda kusali katika ushirika huo na kuwataka waombolezaji wamuombee katika safari yake ya mwisho.

Giyo alisema kuna tabia kwenye jamii na zinafanywa na watu. Yesu aliwaonya Israel kuua watu wake.

Alisema waliofanya mauaji hayo Mungu atakwenda kushughulika nao na kuwaomba wafiwa wasilie katika kipindi hiki kigumu wanachopitia na waendelee kumuombea marehemu.

"Kuna watu ambao tabia zao haziishi katika jamii kama una tabia mbaya ama kuua watu acha hiyo tabia kuna msemo asiyesikia la mkuu... kama upo miongoni mwa watu unawasema vibaya wenzako kama ni ofisini acha, kama una tabia ya kuua watu kwa maneno acha hiyo tabia," alisisitiza Giyo na kuongeza.

"Kuna watu wanafanya utajiri wa mtu kama mali yao, Biblia inasema kila mtu apandacho ndio atakachovuna kifo cha Jonson kitufundishe kuishi kwa matendo mema," alisema.

Mwajiri wa Vodacom, Ester Masala, alisema wamempoteza mtu muhimu, alikuwa mchapakazi na mwenye upendo kwa wenzake.

Alisema kifo chake kimewashtua na wataendelea kumuombea pamoja na familia yake.

Maziko yake yamefanyika katika makaburi ya Ununio jana, majira ya saa 10 alasiri.

TRA

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## HAKI NA WAJIBU WA MLIPAKODI

### HAKI

1. Kusikilizwa na Kuhudumiwa bila upendeleo
2. Kupewa fursa ya kuaminiwa
3. Haki ya kuwasilisha malalamiko au pingamizi la makadirio
4. Kutatuliwa malalamiko na kupewa majibu ya maulizo yako kwa wakati

### WAJIBU

1. Kulipa kodi au ushuru kabla au mnamo tarehe ya mwisho ya kulipa kodi husika
2. Kutuma ritani za kodi katika kipindi kilichowekwa kisheria
3. Kutunza kumbukumbu za biashara, kutoa na kudai risiti katika mauzo na manunuzi
4. Kutoa taarifa za maandishi TRA pindi unapofunga biashara yako

Kwa maelezo zaidi, piga simu bure; 0800-780078 au 0800-750075,
WhatsApp: 0744-233 333 Barua pepe: huduma@tra.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongereni Simba kiwango bora CAF, jipangeni upya

**SAFARI** ya wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya kimataifa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika imefikia ukingoni licha ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Ushindi huo haukutosha kwa Simba kuweza kupindua matokeo kutokana na mechi ya mkondo wa kwanza iliyopigwa Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini, kukubali kipigo cha mabao 4-0, hivyo ilikuwa ikihitaji angalau kushinda 5-0 ama zaidi ili kutinga nusu fainali ya michuano hiyo.

Kwa ujumla, tunaipongeza Simba kwa matokeo iliyoyapata juzi na zaidi kwa kiwango ilichokionyesha katika mechi zote hususan hatua hiyo ya robo fainali ambayo walishindwa kusonga mbele licha ya ushindi huo.

Tukiwa kama wadau wakubwa na namba moja wa michezo nchini, licha ya kutambua kwamba mpira wa miguu una matokeo matatu; kushinda, kushindwa na sare, lakini pia tunatambua mara nyingine soka huwa lina matokeo ya kikatilii, ambayo ni vigumu kuyapokea na ndiyo yaliyoikuta Simba.

Tunasema hivyo, hasa tukizingatia kwamba, tangu kuanza kwa michuano hiyo msimu huu, Simba ni moja kati ya timu iliyokuwa ikipewa nafasi kubwa ya kufika fainali kutokana na kiwango kikubwa ilichokionyesha tangu mwanzo.

Katika mechi 12 ilizocheza hadi kutolewa, imepoteza michezo miwili pekee, bao 1-0 dhidi ya FC Platinum katika kuwania kufuzu hatua ya makundi na 4-0 dhidi ya Kaizer Chiefs hatua ya robo fainali, mechi zote ikipotezea ugenini na ikishinda zote za nyumbani.

Kwanza ilianza kuitoa Plateau United ya Nigeria baada ya kushinda bao 1-0 ugenini kisha kutoka sare tasa nyumbani, na baadaye ikafungwa 1-0 ugenini na FC Platinum ya Zimbabwe kabla ya nyumbani kushinda 4-0 na kuitoa katika michuano hiyo, hivyo kutinga hatua ya makundi.

Simba ambayo ilipangwa Kundi A, ilianza kwa kuichapa AS Vita ya DR Congo kwao bao 1-0, kisha ikapata ushindi kama huo dhidi ya bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri na baadaye ugenini kutoka sare tasa dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan.

Mechi ya marudiano katika Uwanja wa Mkapa, Simba ikaichapa Al-Merrikh 3-0 na kisha ikaifumua AS Vita mabao 4-1 hapa nchini kabla ya kwenda Misri kuhitimisha hatua ya makundi ambapo ilipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Al Ahly.

Hicho ni kiwango cha juu kabisa kuwahi kuonyeshwa na timu kutoka ukanda huu wa Afrika Mashariki katika michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, hivyo wanachama, mashabiki Simba, viongozi wa klabu hiyo pamoja na Watanzania kwa ujumla, hawana budi kujivunia na kuwapongeza wachezaji kwa kiwango bora kabisa kilichoonyeshwa na wawakilishi hao wa nchi kimataifa.

Tunaamini Simba imetoa onyo katika michuano hiyo, kwa timu ambazo msimu ujao zitapangwa nayo, hivyo huu ni wakati wa viongozi wa klabu hiyo kushikamana na kuijenga zaidi kwa kuimarisha idara ambazo zimeonekana kuwa dhaifu kuelekea msimu ujao.

Kwa ujumla wachezaji na benchi la ufundi, hawana deni kwa viongozi wa klabu hiyo, kwani wametimiza malengo waliyokuwa wamewekewa awali ya kufika robo fainali, hivyo deni lao kwa sasa ni kutimiza malengo mengine ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA ili kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Tunaamini kama Simba itajipanga vema kwa kuimarisha kikosi chake na kubaki na benchi lake la ufundi, itafika mbali zaidi msimu ujao na kuwa fahari na nembo ya soka la Tanzania kimataifa katika ngazi ya klabu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi Ligi Bara wamepoteza umakini mwishoni

**NI** kama vile kuna mpango wa kuzibeba baadhi ya timu hasa kuelekeza mwishoni mwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Hivi ndivyo inavyoonekana kwa baadhi ya mashabiki wa soka baada ya kushuhudiwa matukio kadhaa yasiyo ya kawaida kwenye mechi za hivi karibuni.

Kwa sasa inaonekana kadri Ligi Kuu Tanzania Bara inavyoelekea ukingoni, ndipo umakini wa waamuzi na wasaidizi wao unavyozidi kupungua. Haijulikani kama ni makusudi au bahati mbaya, lakini inaonekana kuwatia shaka wadau wengi wa soka.

Aprili 24, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Gwambina, Simba ilipokuwa inacheza na Gwambina FC, kwa mastaajabu ya wengi, mwamuzi msaidizi Godfrey Msakila alikataa bao la Joash Onyango alipounganisha kwa kichwa mpira wa kona uliopigwa na Clatous Chama na hadi leo hakuna anayejua hasa sababu ya kukataa bao lile.

Mei 15, mwamuzi msaidizi mwingine, Abdulaziz Ally alikataa bao la Yanga lililofungwa na Yacouba Sogne akiunganisha mpira wa kona uliopigwa na Saido Ntibazonkiza kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi. Lilifanana vile vile kama lile la Simba. Waamuzi wote hao wamepewa adhabu ya kuondolewa kwenye mizunguko mitatu ya ligi, lakini tayari timu zimeshaumia.

Baada ya kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera Mei 17, Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire alimshukia mwamuzi Abdallah Mwinyimkuu kwa kile alichodai hakuwatendea haki na aliwabeba kwa mbeleko ya chuma wenyeji ili wapate ushindi kwa lazima.

"Mwamuzi Mwinyimkuu hakututendea haki. Ni kama aliwabeba wenyeji. Angalia kwanza tukio la daktari wa Kagera Sugar kumsukuma mchezaji wetu, mwamuzi hakuna lolote alilofanya. Hakuna hatua yoyote aliyochukua. Wachezaji wetu Said Nyoso na Zuberi Dabi, walipewa kadi za njano bila sababu yoyote ya msingi na hii ilikuwa ni mpango tu wa kuwatoa mchezoni," alisema Masau.

Alisema anaamini Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB) wanataka nchi iwe na ligi bora, lakini baadhi ya waamuzi wamekuwa wakikwamisha hilo na kusababisha malalamiko mengi kwenda kwao bila sababu yoyote.

"Watu wanawaona kama TFF hawafai kwa sababu ya waamuzi wa aina hii. Na si kwamba hakuna waamuzi wazuri. Wapo na hata sisi viongozi wa klabu tunawajua waamuzi wazuri wakitaka tutawasaidia kuwataja, lakini hawa wengine ni matatizo matupu. Tunaingia gharama, tunajiandaa, lakini tunakwamishwa na watu wachache kwa manufaa yao," alisema Masau.

Siku tatu baadaye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata, alimlalamika vikali mwamuzi wa mchezo kati ya timu yake dhidi ya Ihefu, Ludovic Charles, kuwa aliwabeba wapinzani wao kwa mbeleko ya chuma na yeye ndiye aliyekuwa nyota wa mchezo huo, timu yake ikipoteza kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Highland Estate, Mbarali, mkoani Mbeya.

Makata alisema hayo mara baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake ya Dodoma Jiji ambayo ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Ihefu.

"Kusema kweli tumepoteza, lakini nyota wa mchezo alikuwa refa. Lazima tuseme ukweli, penalti haikuwa sahihi na kakataa mabao mawili ambayo ni sahihi. Hii yote ni kutaka kuwatoa kwenye mchezo. Lakini nashukuru wachezaji wangu hawakutoka mchezoni, walichokuwa wanakikosa ni umakini tu wa kumlaizia nafasi," alisema kocha huyo na kuonya.

"Hizi mechi za mwisho lazima tuwe makini sana. Beki wangu hakushika, refa atapewa adhabu, lakini sisi tunakuwa tumeshapoteza mechi, hii ni mbaya sana."

Marudio ya mechi hiyo yanaonyesha kuwa mpira ulimgonga tumboni beki mmoja wa Dodoma Jiji, huku mikono akiwa ameiweka nyuma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Sudi Abdi kwa upande wake amesema kuwa malalamiko kwenye Ligi Kuu hasa kuelekea mwishoni mwa msimu yapo, lakini yanakwenda kwenye kamati husika, yatajadiliwa na kama yana ukweli basi yatatolewa maamuzi.

"Siwezi kuingilia, kamati itafanya kazi yake na itachukua hatua. Makosa yanaonekana. Hakuna mwamuzi ambaye hakosei, ila yakizidi na kuleta athari kubwa yanachukuwa hatua. Lakini nawataka tu waamuzi kuzidisha umakini kwa sababu ligi inaelekea ukingoni ili kila timu ivune ilichokipanda," alisema mwamuzi huyo wa zamani.

MAKALA MAALUM

# NHC kuanza kunufaisha watu wa kipato cha chini

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa kipato cha chini nchini wataanza kunufaika na nyumba za gharama nafuu kufuatia mpango uliobuniwa na Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) wa kuanza kuzalisha vifaa vyake vya ujenzi kuanzia mwaka ujao wa fedha.

NHC ambayo ilianzishwa mwaka mmoja baada ya uhuru, ikiwa ni miongoni mwa mashirika ya umma ya kwanza nchini, ilianza kwa kutekeleza kile kilichoitwa 'operesheni ondoa makuti' jijini Dar es Salaam kwa kujenga nyumba za gharama nafuu. Kazi hiyo baadaye ilihamia katika miji mingine.

Hata hivyo, kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi kulionekana kukwamisha mpango wa ujenzi wa nyumba hizo. Shirika hilo sasa limepanga kujenga nyumba katika kila wilaya, lakini limekuwa likikumbana na vikwazo kama bei ya juu ya saruji, mabati, kokoto na vifaa vingine ambavyo husababisha kupanda kwa gharama ya nyumba hizo.

Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, anasema shirika hilo linaandaa mitambo kwa ajili ya kuzalisha vifaa vya ujenzi kuanzia mwaka 2021/22.

Kwa kuanzia, mitambo ya viwanda hivyo inaanzia kusimikwa jijini Dodoma na baadaye kuelekezwa kwenye maeneo mengine nchini.

"Kwa watu wenye kipato cha chini, gharama ya nyumba inapaswa kuwa kati ya Sh. milioni 10 na 20, lakini gharama ya juu ya vifaa hufanya nyumba hizo na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kufikia bei ya Sh. milioni 40 hadi milioni 55," alisema Saguya.

Alisema, bei ya nyumba zilizojengwa katika mradi wa majaribio uliohusisha wilaya 34 ilikuwa juu kwa kuwa NHC ililazimika kununua ardhi na kujenga miundombinu ya kuhudumia maeneo hayo kama vile maji, umeme, barabara na mitaro ambavyo vinapaswa kutekelezwa na mamlaka nyingine husussan TANESCO, TARURA na nyingine.

"Tulijenga nyumba 1,300 chini ya miradi ya awali ya gharama nafuu, lakini bei ya kuuzia ilipanda na kufanya baadhi ya halmashauri za wilaya na manispaa kushindwa kulipa," alisema.

Uwezo mdogo wa kifedha kwa wananchi walio wengi umeifanya NHC kubadilisha sera yake ya kuuza asilimia 70 ya nyumba zake ilizojenga na kupangisha zilizobaki. "Hivi sasa tunauza asimilia 20 tu ya nyumba na asilimia 80 tunapangisha," alifafanua.

Msisitizo wa NHC kwa sasa ni kujenga nyumba za gharama nafuu, ingawa mpango huu utaenda sambamba na miradi mingine itakayowalenga watu wa kipato cha kati na juu. Miradi hiyo itasaidia pia kufidia gharama za nyumba nafuu.

Hivi sasa NHC inawekeza kwenye miradi ya miji pembezoni ya Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Dodoma, ambako inajenga nyumba 1,000 kwa ajili ya watumishi wa serikali waliohamishiwa kwenye makao makuu mapya ya nchi. Kiasi cha Sh. bilioni 70 zimewekezwa katika mradi huo wa Dodoma utakaojengwa kwa awamu tatu, kwa mujibu wa Saguya.



Mwonekano wa nyumba za gharama nafuu 300 zinazoendelea kujengwa Iyumbu, ambazo zitauzwa na kupangishwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Miradi mingine inayotekelezwa ni wa Golden Premier Residences, Morocco Square na Kawe 711, Mkoa wa Dar es Salaam. Pia, Morocco square imekamilika ujenzi wake kwa asilimia 95.

NHC pia ilipewa kandarasi ya kujenga machinjio ya Vingunguti, Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,000 na mbuzi 500 na kondoo 500 kwa siku, na hospitali za rufaa katika miji ya Musoma na Mtwara.

Pia inajenga nyumba za makazi 44 kwa ajili ya wafanyakazi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Shirika hilo linaamini kuwa utaratibu unaotumika wa utoaji wa mikopo ya nyumba utawawezesha watu wengi zaidi kununua nyumba. NHC imekaribisha benki 19 kujiunga katika mpango huo, ambao umetoa mikopo ya Sh. bilioni 20 hadi sasa, ingawa masharti yake hayajawa rafiki sana.

Benki ya Dunia pia imekuwa ikisaidia kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wajenzi kupitia Benki Kuu na Kampuni ya Tanzania Mortgage Refinancing (TMRC).

Mahitaji ya nyumba nchini Tanzania ni milioni tatu kwa mwaka na yamekuwa yakiongezeka kwa nyumba 200,000.

Wataalamu wa sekta ya ujenzi na wadau wanasema serikali inapaswa kuunda sera madhubuti ya kuongoza sekta hiyo yenye mchango mkubwa kwa uchumi wa taifa.

Wadau pia wanashauri kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye vifaa vya ujenzi ili kupunguza gharama. Pia wanataka tozo nafuu kwenye mauzo ya vifaa hivyo ili kuunda mfuko maalum utakaosaidia ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, kama ilivyo kwa mfuko wa barabara na mifuko mingine.

# LHRC yajitosa sakata la watoto wa kike kutoroshwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimefanya ziara ya kuitembelea Shule ya Sekondari Itope wilayani Mbeya mkoani Mbeya ambayo wanafunzi wawili wa kike wa kidato cha pili walishatoroshwa na mfanyabiashara mmoja kwa zaidi ya miezi mitano sasa na hawajulikani waliko.

Wanafunzi hao (majina tunayahifadhi) wanadaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara tangu Januari mwaka huu ambapo taarifa ziliripotiwa Polisi kwa RB namba KY41/RB/07/2021 na ISK/RB/41/2021, lakini hadi sasa mtuhumiwa hajakamatwa.

Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, aliongoza wataalamu wa sheria kutembelea shule hiyo na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Shule na mwalimu wa nidhamu na malezi wa shule hiyo ambao walimweleza kuwa wanasikitika wanafunzi hao kusitisha masomo kutokana na kutoroshwa.

Walimu walimweleza Henga kuwa, wanafunzi hao ni muhimu wakapatikana na kurejea kuendelea na masomo, kwani Novemba mwaka huu wanatakiwa kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili.

Aidha, Mkurugenzi wa LHRC alifanya mazungumzo na wazazi, askari wa kituo cha polisi Kyela mjini ambako taarifa za kutoroshwa wanafunzi hao ziliripotiwa kisha kufanya mazungumzo na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei.

Henga aliwaeleza viongozi wa Jeshi la Polisi, walimu na wazazi kwamba LHRC itahakikisha inatoa ushirikiano wa kisheria ili kuhakikisha haki inatendeka katika suala hilo.

"LHRC haifurahishwi na kutoroshwa kwa wanafunzi hao ambao wamesitishiwa ndoto zao za baadaye, tunaliomba Jeshi la Polisi na wadau wengine wasaidie kukamatwa kwa mfanyabiashara aliyewatorosha ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yake," aliesema.

Mzazi wa wanafunzi hao, Simon Mwasitu alisema tukio hilo lilishamkatisha tamaa, kutokana na Jeshi la Polisi kuchukua muda mrefu bila kumkamata mtuhumiwa.

"Mwanangu ana miezi mitano sasa sijamuona na sijui kama yupo hai au amekufa, kila nikienda Polisi naambiwa hajakamatwa, nimekata tamaa, maana hivi sasa maisha yangu yako hatarini kutokana na kuendelea kufuatilia suala hili ambapo wakati mwingine nafungiwa mlango usiku kwa kufuli kwa nje na watu wasiojulikana," alisema.

Mwasitu alisema ujio wa mkurugenzi wa LHRC ni faraja kwao, na kwamba wana imani sasa haki inakwenda kutendeka tofauti na mwanzo, ambapo walikosa imani kutokana jinsi suala hilo lilivyokuwa likiendeshwa.



Mkuu wa Ndaki ya Sayansi ya Afya Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Ipyana Mwampagatwa, akizungumza na wanafunzi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa elimu ya ujasiriamali, mafunzo hayo yalifanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki . **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# World Vision yakumbuka waliokumbwa mafuriko

**Na Restuta Damian,** MISENYI

BAADHI ya wananchi waliokumbwa na mafuriko katika Kata ya Kasambya, wilayani Misenyi, mkoani Kagera, wamepatiwa msaada wa vyakula na vifaa vya malazi.

Msaada huo ulitolewa kwa wananchi hao mwishoni mwa wiki na Shirika la World Vision.

Wananchi hao walikumbwa na mafuriko na kuhifadhiwa na kambi za Shule ya Msingi Kasambya na Kanisa Katoliki tangu Aprili 25, mwaka huu.

Mafuriko hayo yaliharibu nyumba, vifaa vya ndani na mazao shambani.

Mmoja wa wananchi hao, Paschal Barnaba, alisema hajui ni lini atarudi nyumbani kwake kwa kuwa makazi yao bado yamejaa maji mpaka sasa.

Frolida anayeishi kambi ya kanisa hilo, alisema mvua iliyonyesha imeathiri mazao yao na kwamba hajui akirudi atapata wapi chakula.

Mkazi mwingine Amos Edward, alisema; "Mimi ninaomba serikali na haya mashiriki waendelee kutoa misaada tunaona hali hii itaendelea hadi mwezi Desemba na mazao tuliyolima shambani maji yameharibu hatuna uhakika wa kupata vyakula," alisema.

Meneja wa World Vission, Juliana Charles, alisema kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi wametoa Sh. milioni 81.6 kwa ajili ya kununua chakula, blanketi, vyandarua, dawa za kutibu maji na mipira kwa ajili ya kuchezea watoto.

Akizungumzia mafuriko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Misenyi, Innocent Mkandara, alisema kata nne zenye watu 1,277 zimeathiriwa na mafuriko.

## Shule binafsi zatakiwa kuweka ada himilivu

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE binafsi zimetakiwa kupunguza ada ili ziwe himilivu kuwawezesha wazazi wengi wamudu kupeleka watoto wao.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri Ofisi ya Rais ( TAMISEMI), David Silinde, wakati akizungumza kwenye mahafali ya 13 ya Shule ya Sekondari ya St Anne Marie Academy mkoabi Dar es Salaam.

Alisema hatua ya shule hizo kuweka ada himilivu kutatoa fursa kwa Watanzania wengi kupeleka watoto wao kwenye shule hizo, hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa juhudi zinazofanywa na serikali .

"Niwaombe na nyinyi St. Anne, ingawa mnafanya vizuri kitaaluma isiwe kigezo cha kuweka ada isiyohimilivu na kuwashinda wazazi kuleta watoto wao hapa, naomba muwe na utu kwa kuweka viwango rafiki," alisisitiza

Aidha, Silinde alisema mafanikio ya shule hiyo ni matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na walimu na mwanzilishi wa shule hizo, Jasson Rweikiza, pamoja na usimamizi mzuri wa wasimamizi wa elimu Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ubungo.

"Nawasihi wanafunzi mnaohitimu leo muendelee kuwa na nidhamu na tabia njema huko muendako na msiache kusoma kwa bidii kama mlivyokuwa mnafundishwa hapa na nimatumaini yangu kuwa mtajiunga na vyuo vikuu ndani na nje ya nchi,".

Aliipongeza shule hiyo kwa kufaulisha vizuri kidato cha nne mwaka 2020 ambapo wanafunzi 43 walifaulu kwa daraja la kwanza, wanafunzi 63 daraja la pili na wanafunzi 19 daraja la tatu.

"Nimeambiwa kuwa kwenye matokeo ya kidato cha sita mwaka jana pia mlifanya vizuri sana kitaaluma ambapo wanafunzi 19 walipata daraja la kwanza, wanafunzi 47 daraja la pili na 19 daraja la tatu, haya ni mafanikio makubwa sana nawapongeza ila msibweteke," alisema Silinde.

# WanaCCM Morogoro watakiwa kuacha majungu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Morogoro, wametakiwa kuacha majungu badala yake wafanye kazi zenye kuleta maendeleo kwa mawanchi kwa kutekeleza ilani cha chama chao.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho taifa, Daniel Chongolo, aliyeambatana na Naibu Katibu Mkuu Bara, Christina Mdeme, pamoja na Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamidu Shaka, wakati wakijitambulisha.

Chongolo alisema wapo baadhi ya wanachama wamekuwa wakitumia muda mwingi kufanya majungu badala ya kufanya kazi ya kutekeleza ilani ya chama na kuwataka kuachana na tabia hiyo na badala yake wafanye kazi vizuri.

"Lengo la chama chetu ni kutekeleza ilani ya chama chetu kwa manufaa ya wananchi wote katika suala zima la kuleta maendeleo hivyo hatamvumilia mtu atakayeendekeza majungu na fitina ndani ya chama chetu," alisema Chongolo.

Alisema wananchi wanakabiliwa na changamoto nyingi na kwa kuwa CCM imepewa ridhaa ya kuongoza taifa, kila mwanaCCM anatakiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikicha changamoto zote zilizopo katika jamii zinatatuliwa haraka.

Alisema Mkoa wa Morogoro umejaliwa kuwa na rutuba inayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali na alitaka ardhi hiyo itumike vizuri kwa uzalishaji wa mazao na kuepuka migogoro ya ardhi.

Pia alisema changamoto ya barabara ya Mikumi Ifakara hadi Malinyi ameichukua na kuahidi kuanza kuifanyia kazi kuanzia sasa na vijiji vyote ambavyo havina huduma ya umeme ni lazima vipate huduma hiyo.

"Viongozi wa chama tunatakiwa kisimamia miradi yote ya maendeleo na kama kutakuwa na dosari ya aina yoyote tunatakiwa kushauri nini cha kufanya na siyo tu kunyoosheana vidole kwani lengo letu ni kuisimamia serikali," alisema Chongolo.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Mdeme, ambaye pia ni mlezi wa chama mkoa huo aliwataka wanachama kumuunga mkono kwa dhati Rais Samia Suluhu Hassan na ni wajibu wa kila kiongozi wa chama kutatua kero kwa jamii.

Alikemea urasimu kwa wawekezaji na kutaka serikali ihakikishe inaweka mazingira mazuri ya wawekezaji katika mkoa huo ambao wataleta tija katika maendeleo kwa wananchi wote wa Morogoro na taifa zima kwa ujumla.

Alimpongeza Doroth John Mwasansu kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama ngazi ya mkoa na kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Kwa upande wake, Doroth, aliwapongeza viongozi hao kwa kuteuliwa na Rais Samia na kuahidi kuwapa ushirikiano.



Mwanafunzi wa kidato cha tano Shule ya Sekondari St Anne Marie Academy ya Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, Cecilia Kadonyi. akionyesha namna pombe kali inavyoweza kuharibu maini kwenye Mahafali ya 13 ya kidato cha sita yaliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 'Uoto Mlima Kilimanjaro lazima ulindwe'

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesisitiza uoto wa asili wa Mlima Kilimanjaro unapaswa kulindwa ili kuufanya uendelee kuwa kivutio kwa watalii wengi.

Jafo alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao kifupi na Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Stephen Kigaigai, katika ziara yake ya kikazi mkoani humo kwa ajili ya kukagua uzingatiaji wa hifadhi ya mazingira. Alisisitiza serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) inaendelea kusimamia uhifadhi wa mazingira nchini kwa maslahi mapana ya nchi.

Mkuu wa Mkoa huo, Kigaigai alimhakikishia Waziri Jafo kwamba atahakikisha juhudi za serikali za kulinda mazingira anazisimamia ipasavyo katika mkoa huo.

Katika ziara hiyo, Jafo alitembelea dampo la kisasa katika Manispaa ya Moshi, akiwapongeza viongozi na watendaji wa manispaa hiyo kwa namna wanavyohifadhi taka ngumu zinazozalishwa kila siku katika manispaa hiyo.

Akikagua shughuli zinazofanyika katika dampo hilo, waziri huyo alifurahishwa na namna wataalamu wanavyosimamia vyema utupaji wa taka hizo sambamba na ubadilishaji wa baadhi ya taka hizo kuwa mboji. Kutokana na hali hiyo, alizitaka halmashauri zingine nchini kuiga mfano wa manispaa hiyo katika uhifadhi bora wa taka ngumu. Waziri huyo pia alitembelea kiwanda cha China Paper Industry na kuwataka wamiliki wa kiwanda hicho kutafuta njia ya kutumia nishati mbadala kwa kuwa kwa sasa wanatumia magogo mengi kwa ajili ya nishati na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Aliwapa mwaka mmoja wamiliki wa kiwanda hicho kuja na njia nyingine ya nishati mbadala wa magogo yanayotumika sasa ili kuepusha ukataji wa miti ovyo.

Waziri huyo pia aliwataka wamiliki wa kiwanda cha kutengeneza nondo cha Five Star Steel kinachotumia chuma chakavu kuepuka kununua vyuma vinavyotoka katika miundombinu ya umma ikiwamo madaraja, alama za barabarani na kutoka kwa watu binafsi ili kutoleta hasara kwa jamii. Jafo alikipongeza kiwanda hicho kwa kudhibiti kusambaa kwa moshi katika kiwanda hicho ambapo kwa siku za hivi karibuni uliripotiwa kuwa kero kwa raia wanaoishi jirani ya kiwanda hicho.

## Ushirika wawalipa wakulima wa pamba

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

VYAMA vikuu vya ushirika vya Kahama (KACU) na Chato (CCU) vimewalipa wakulima wa pamba jumla ya Sh.milioni 90.6.

Hayo ni malipo ya pili baada ya vyama hivyo kupata faida kutokana na uwezeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Pia ni mara ya kwanza vyama hivyo kuwalipa wakulima mara ya pili katika kipindi cha miaka 15, na hatua hiyo inatokana na jitihada za benki hiyo katika kulifufua zao hilo, baada ya kuwekeza pia katika viwanda vya kuchambua pamba pamoja na kutoa pesa ambazo ziliwezesha ununuaji wa zao hilo.

Meneja wa TADB Kanda ya Ziwa, Mike Granta, alisema malipo hayo ya pili ni sehemu ya jitihada ya pamoja ya kunyanyua pato la mkulima na kuinua uzalishaji wa pamba hapa nchini.

"Benki tunafanya kazi kwa karibu na vyama hivi vya Chato na Kahama katika kuhakikisha tunaongeza matumaini na ari ya wakulima wa pamba na hatimaye kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa zao hili la kimkakati," alisema Granta.

Amesema benki kwa kushirikiana na vyama hivyo wamekarabati viwanda viwili vya kuchambua pamba kwa gharama ya Sh. bilioni 1.2, hivyo kusaidia kuongeza kasi ya uzalishaji wa pamba.

"Benki ilifufua kiwanda cha KACU pamoja na cha CCU kama sehemu ya mkakati wa kuinua uzalishaji wa zao la pamba na kulifanya zao hili liongeze mchango katika pato la taifa," alisema Granta.

Aliongeza kuwa benki hiyo iliwezesha upandishaji wa bei ya pamba kutoka Sh. 810 iliyokuwa imepangwa na Bodi ya Pamba hadi kufikia Sh. 950 kwa kilo, baada ya kuwekeza Sh. bilioni 11 katika eneo hilo na kufafanua kwamba baada ya tukio hilo hata wanunuzi wangine wakapandisha bei kufikia Sh. 900 kwa kilo.

"Kwa msimu uliopita benki kwa kushirikiana na vyama hivi vya ushirika tulitumia jumla ya Sh. bilioni 11 kuratibu shughuli mbalimbali za vyama hivyo ikiwamo ukarabati wa viwanda pamoja na ununuzi wa pamba. Hata hivyo kutokana na uchache wa pamba kwa msimu uliopita, vyama vilitumia Sh. bilioni 7.6," alisema na kuongeza kuwa kwa pamoja sasa wanafanya jitihada zaidi ili uzalishaji uongezeke msimu ujao.



Meneja Kilimo wa Tanzania Breweries Limited (TBL), Joel Msechu (kulia), akiongea na wakulima wa mtama wanaoshirikiana na kampuni hiyo wakati walipotembelea shamba la mtama la mfano wakati wa maonyesho ya TARI yaliyofanyika Hombulu mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki, TBL imedhamini wakulima kushiriki maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA yatoa elimu mabadiliko ulipaji bili

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeendelea kutoa elimu kwa wateja wake wa Dar es Salaam na Pwani juu ya mabadiliko ya usomaji wa mita za maji na upokeaji wa bili za maji yaliyofanywa hivi karibuni.

Mabadiliko hayo yanahusisha usomaji wa mita yaliyofanywa na mamlaka hiyo kutoka tarehe 1 hadi 15 kwenda tarehe 20 hadi 30 ya kila mwezi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti juu ya mabadiliko hayo, wakazi wa Dar es Salaam na Pwani walipongeza mabadiliko hayo na kusema yamefanyika wakati mwafaka na yataleta tija kwa mamlaka na wananchi kwa ujumla.

"Tunaishukuru DAWASA kwa mabadiliko haya ya usomaji mita kwa tarehe za mwisho wa mwezi, sisi wananchi tulishasema sana kuhusu kuletewa bili tarehe tofauti tofauti wakati vipato vyetu vinatofautiana," alisema Ramadhan Abdul, mkazi wa Kinondoni Shamba.

Zakia Mrisho, mkazi wa Kitongoji cha Sanze, Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, alisema mabadiliko hayo yatasaidia wananchi wanaotegemea vipato vyao mwisho wa mwezi.

"Mfano sisi watumishi wa umma kipato chetu kikuu ni mshahara unaolipwa mwisho wa mwezi, DAWASA walivyokuwa wanatusomea bili na kutuma meseji muda wowote halikuwa jambo zuri, tuliishia kugombana nao na wakati mwingine kutoleana vitisho mbalimbali.

"Lakini kwa mabadiliko haya tunajua wamesikia kilio chetu na wakaamua kujirekebisha," alisifu.

Mkurugenzi wa Biashara na Huduma kwa Wateja DAWASA, Rithamary Lwabulinda, alisema mabadiliko hayo yaliyofanywa na mamlaka, yalifanyiwa utafiti wa kina na shirikishi kwa lengo la kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

"Mara kwa mara huwa tunatenga muda wa kuongea na wateja wetu, hivyo mabadiliko haya ni miongoni mwa sauti za wateja wetu walizotushauri juu ya uboreshaji wa huduma zetu ili kuwafikia wengi zaidi," alisema.

# Wanafunzi kilimo wapewa fursa mafunzo kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa kilimo wamepewa fursa ya masoko viwandani ili kuimarisha sekta ya kilimo.

Fursa hiyo imetolewa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) ukiwa ni mwendelezo wa kuwapa fursa wanafunzi wa taaluma ya kilimo kujifunza kwa vitendo.

Kampuni hiyo ilitoa nafasi kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo na Mifugo cha Kilacha kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro kutembelea kiwanda chake kilichopo Moshi mjini.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema, programu ya Kilimo-Viwanda inawajengea wanafunzi wa kilimo uwezo wa kuelewa kwa vitendo. Kupitia ziara hii wanafunzi wamejionea namna malighafi za mashambani zinavyotumika kutengeneza bia". Ocitti alifafanua kuwa ufadhili chini ya kilimo viwanda unajumuisha malipo yote ya chuo na gharama zingine katika kipindi chote cha masomo kwa wanafunzi wanaochaguliwa, na kuongeza kuwa programu hiyo inawalenga wanafunzi wanaotoka katika familia maskini ambazo haziwezi kumudu kugharamia masomo kwa watoto wao.

Alisisitiza kuwa program hiyo imelenga kusaidia juhudi za serikali kuongeza idadi ya maofisa kilimo. "SBL ni mzalishaji wa bia mkubwa nchini kwa kutumia nafaka za ndani katika utengenezaji wa bia. Hadi sasa SBL inafanya kazi na mtandao wa wakulima 400 kwenye mikoa nane nchini ambapo tunanunua nafaka kama shayiri, mahindi na mtama kwa ajili ya uzalishaji bia. Inatumia takribani tani 17,000 sawasawa na asilimia 70 na mahitaji yao kwa mwaka." alisema

Programu ya ufadhili wa masomo ya Kilimo Viwanda ilianzishwa mwaka 2020 na jumla ya wanafunzi 71 wamenufaika nayo kwa kupata fursa ya kusomea kozi za diploma ya kilimo katika vyuo vingine vitatu ambavyo ni Kaole Wazazi College of Agriculture (Bagamoyo), cha Igabiro Training Institute of Agriculture (Bukoba) na St. Maria Goretti Agriculture Training Institute (Iringa).

Katika upande wake, Meneja Msaidizi wa Chuo hicho, Padre Jerome Silayo, aliipongeza SBL kwa msaada wao wa katika kusaidia maendeleo ya kilimo na kuzitaka kampuni nyingine kuiga mfano katika kuwasaidia wanafunzi kutoka familia masikini nchini.

# Waomba maeneo ya kulima alizeti

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wasindikaji Mafuta ya Alizeti Tanzania (TASUPA), kimeiomba serikali itoe maeneo ya kilimo cha zao hilo nchini kote, kukabiliana na uhaba ikiwamo bei kubwa ya mafuta iliyopo sokoni hivi sasa.

Kimesema mbali na serikali kutenga maeneo hayo kwenye baadhi ya mikoa, bado hayatumiki kwa shughuli ya kilimo hicho.

Mwenyekiti wa TASUPA, Ringo Iringo akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye moja ya kipindi kinachorushwa na kituo cha ITV, alisema kilimo kinachofanywa hivi sasa na wakulima wa zao hilo, hakina tija.

"Kilimo cha alizeti kwa wakulima wengi ni kama mazoea tu si rasmi, utakuta kwenye shamba la mahindi ndio inalimwa alizeti chache tu. Yawepo maeneo na mashamba rasmi ili kukabiliana na kupanda bei na uhaba wa mafuta ya kupikia," alisema Iringo."

"Serikali itoe maeneo ya kilimo cha mazao yanayozalisha mafuta. Hivi sasa tunapata hasara, hakuna mbegu za kukamua mafuta ili yasindikwe."

Alisema hivi sasa kuna viwanda viwili pekee vya alizeti nchini vinavyoendelea na uzalishaji, vingine vikifungwa kutokana na uhaba wa malighafi na kwamba wanatarajia wiki hii vitafunguliwa kutokana na mavuno ya mbegu kuongezeka.

"Uzalishaji alizeti umeanza ndio utaona viwanda vingine vinaanza kufunguliwa.

Mfano kiwanda kimoja uwezo ni kuwa na tani 100 za alizeti ili kukamua, hakuna mkulima anazalisha kiasi hiki. Viwanda vingi vinasuasua," alisema Iringo.

Iringo akiongeza kwamba, tatizo hilo limechangia uhaba wa ajira na uwekezaji kushuka na kwamba mafuta hayajaadimika kwa mahitaji ya majumbani pekee, bali hata viwandani ambako yanahitajika ili kusindikia vyakula mbalimbali.

Aliongeza kwamba viwanda 770 vinahitaji zaidi ya Tani 4,000 kwa siku, na havipati na kwamba walikwishatoa wito kwa serikali kuweka mkakati wa kuboresha mbegu bora, tangu mwaka 2016 ingawa bado haujatekelezwa ipasavyo.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe alisema ipo haja ya kujenga uwezo na kuwahamasisha wakulima kulima mazao yanayozalisha mafuta, ikiwamo mchikichi, kwa ajili ya mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali inatambua kuna upungufu wa mafuta ya kula, kutokana na uwezo wa nchi kuwa mdogo katika uzalishaji na kwamba mahitaji ni tani 564,000 kwa mwaka huku uwezo ni 206,000.

Mwambe, akiwa mkoani Tabora, wakati kuzindua kitabu cha mwongozo wa uwekezaji mkoani humo, alisema ipo mikoa ikiwamo Tabora ambayo ina uwezo wa kuzalisha mazao au mbegu za mafuta ikiwamo, pamba, michikichi na kwamba fursa hiyo ikitumika vizuri itainua kiwango cha uchumi wa wananchi na taifa.

"Mafuta ya kula ni muhimu, sasa tujenge uwezo wetu kuhamasisha wakulima kulima mazao yanayotoa mbegu ambazo huzalisha mafuta. Tabora mnazalisha pamba kwa wingi, mchikichi pia, maendeleo ya nchi ni mchakato unaohitaji kuwekeza," alisema Mwambe.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WALIOITENDEA HAKI JEZI NAMBA 9 DIMBANI UK. 12-13

# NYOTA WATANO WALIOFANYA KAZI ZINGINE KABLA YA SOKA



VARDY

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Robert Lewandowski dakika ya 90 wakati Bayern Munich ikishinda 5-2 dhidi ya FC Augsburg limemwezesha kufikisha mabao 41 kwa msimu huu wa Bundesliga, hivyo kuvunja rekodi ya mfungaji bora wa wakati wote kwa msimu mmoja, Gerd Muller ya kufunga mabao 40, iliyodumu kwa miaka 49. Lakini pia hilo ni bao lake la 53 katika mechi 46 za mashindano yote kwa klabu na timu yake ya Taifa ya Poland msimu huu.



**LONDON,** England

WAKATI kila mchezaji anatarajia kufanikiwa katika ulimwengu wa mpira wa miguu, si kila mtu anafanikiwa kufanya hivyo. Mchezo huo mzuri umejaa hadithi za kuanzia kwenye umaskini wa kutupwa hadi utajiri, hasa kwa wachezaji ambao waliendelea kucheza kwa klabu kubwa barani Ulaya.

Lakini wachezaji wengi wanaocheza soka kwenye madaraja ya chini wana kazi mbadala, kwani hawapati fedha za kutosha kucheza mchezo huo. Hiyo ni kweli hasa kwa wachezaji wengi katika daraja la pili au la tatu la mpira wa miguu au wale wanaocheza mpira ambao si wa ligi.

Kumekuwa na visa kadhaa vya wachezaji ambao wamekuwa na kazi mbadala kabla ya kupanda daraja na kuonja mafanikio hapo juu. Kwenye makala haya, tunawaanglia wachezaji watano kama hao, bila mpangilio wowote, shuka nayo sasa...

### #5. CHARLIE AUSTIN (FUNDI MATOFALI)

Charlie Austin alianza kucheza mpira wa miguu ambao si wa ligi mnamo 2006 kabla ya kuingia kwenye soka la ushindani la Uingereza miaka mitatu baadaye. Kabla ya kuichezea Swindon iliyokuwa Daraja la Kwanza, Austin alikuwa akifanya kazi ya kutengeneza matofali ili kupata kula yake.

Hata hivyo, maisha yalibadilika kwa kuwa bora sana kwa nyota huyo ambaye wakati huo alikuwa na umri wa miaka 20. Straika huyo alipanda na kucheza kwenye Ligi Kuu England akiwa na Queens Park Rangers, Southampton na West Bromwich Albion.

Hata hivyo, mchezaji huyo ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 31, hakuweza kuitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa

### #4. IAIN DOWIE (INJINIA WA ROKETI)

Tofauti na wachezaji wengine, Iain Dowie, hakupata shinda kuanza kucheza soka la kulipwa. Kwa sababu straika huyo wa miaka ya 90', ambaye alicheza jumla ya mechi 300 za ligi katika klabu mbalimbali nchini England, alikuwa mwanasayansi injinia wa roketi.

Akiwa na umri wa miaka 54 sasa, alianza kucheza soka lisilo la ushindani kabla ya kutua Chelsea na baadaye Sheffield United. Awali alikataa kuichezea Sheffield ambao walimpa ofa ndogo ya mshahara kuliko aliokuwa akipata kwenye kazi yake ya injinia wa roketi.

### #3. PETER SCHMEICHEL (MFANYA USAFI)

Peter Schmeichel, golikipa bora katika historia ya Manchester United akishinda mataji matatu mwaka 1999. Kabla ya kuingia kwenye soka, Schmeichel alikuwa anafanya kazi kwenye kiwanda na kufanya usafi kwenye vyumba vya wazee.

Gwiji huyo alianza kucheza soka katika klabu ya Hvidovre ya nyumbani kwao nchini Denmark mwaka 1984.

Baadaye akaichezea Brondby, moja ya timu kubwa nchini humo kabla ya kujiunga na miamba wa soka la Uingereza, Manchester United ambayo alijiunga nayo mwaka 1991. Na kuanzia hapo hakuangalia tena nyuma.

Akiwa chini ya kocha Sir Alex Ferguson hapo Man United, Schmeichel alishinda mataji matano ya Ligi Kuu England, matatu ya FA na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #2. MIROSLAV KLOSE (SEREMALA)

Miroslav Klose ndiye mfungaji wa wakati wote wa Kombe la Dunia na ameifungia mabao mengi zaidi Ujerumani kwenye mechi za kimataifa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 42 kwa sasa, alianza kufurahia mafanikio kwenye soka wakati alipoanza kucheza soka la kulipwa mwaka 1998.

Klose alihamia Ujerumani kutoka nchini kwao Poland akiwa na umri wa miaka nane, akiwa hawezi kuzungumza neno hata moja la Kijerumani. Na alikuwa na wakati mgumu wakati wake wa utoto, kwani watoto wenzake majirani zake walikataa kucheza naye mpira wa 'chandimu' kwa sababu hajui lugha ya Kijerumani.

Akiwa na umri wa miaka 16, Klose alifaulu mhitani wake wa kufanya kazi ya useremala na akawa mtu wa safari tu, lakini kumbe maisha yalikuwa na mipango naye tofauti kabisa.

Wakati Klose alipoanza kuichezea klabu yake ya kwanza ya SG Blaubach-Diedelkopf, haraka akaachana na kazi yake na kumpeleka kwenye mafanikio makubwa. Mengine yote yamebaki kuwa historia kwake.

### #1. JAMIE VARDY (MFANYAKAZI KIWANDANI)

Jamie Vardy katika maisha yake hakuwahi kufikiri siku moja atashinda taji la Ligi Kuu England akiwa na Leicester City mwaka 2016.

Leicester City iliweka historia ya kushinda kombe hilo msimu wa 2015-16 na Vardy ndiye akiwa kiungo mkubwa wa mafanikio hayo akiwa amefunga mabao 24. Kikosi hicho kilichokuwa kinanolewa na kocha Claudio Ranieri, hakikutabiriwa kabisa wakati wa kuanza kwa msimu huo kama kitashinda taji hilo, kwani kilipewa pointi moja kati ya 8,000 za kushinda.

Vardy, ambaye alikataliwa kusajiliwa Sheffield United wakati akiwa na umri wa miaka 16, mchana alikuwa anafanya kazi kiwandani na usiku alikuwa akicheza katika timu ya Halifax Town ambayo haikuwa kwenye ligi yoyote ya ushindani.

Baadaye mchezaji huyo ambaye sasa ana umri wa miaka 34, akasajiliwa na Fleetwood, ambako alikuwa mfungaji bora na akasajiliwa na Leicester City wakati huo ilikuwa Ligi Daraja la Kwanza.

Leicester walitoa kiasi cha pauni milioni moja ikiwa ni rekodi ya kutoa fedha nyingi kununua mchezaji kutoka kwa timu isiyo kwenye ligi yoyote mwaka 2012 na kumsajili Vardy.

Baada ya kuisaidia Leicester City kupanda Ligi Kuu msimu wa 2013-14, Vardy akapata zawadi kubwa miaka miwili baadaye wakati walipotwaa taji la Ligi Kuu England.

# WACHEZAJI 10 WALIOITENDEA HAKI JEZI NAMBA 9

**LONDON,** Egland

MABAO ndiyo yanayoleta ushindi kwenye mchezo wa soka. Ukizungumzia ufungaji wa mabao, wachezaji wakubwa wamefanya hivyo wakiwa na jezi namba tisa.

**Kiutamaduni, jezi namba tisa ndiyo inayohusika na ufungaji wa mabao, ingawa soka la kisasa mambo yamebadilika kidogo katika mbinu – lakini kazi ya namba tisa inabaki ile ile ya kucheka na nyavu.**

Kwa maana hiyo, makala haya yanawaangalia wachezaji 10 ambao wameitendea haki jezi namba tisa, twende sasa...

### #10. LUIS SUAREZ

Luis Suarez ni mmoja wa wachezaji wakubwa wanaovaa jezi namba tisa katika historia ya mchezo huo ambaye bado anacheza hadi sasa.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Uruguay ni mmoja wa washambuliaji waliokamilika zaidi katika kizazi chake.

Katika umri wake wa miaka 34, amekuwa na mafanikio makubwa katika klabu alizozichezea; akianza kushinda taji la Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, akiwa na Ajax, Kombe la Ligi na Liverpool, kabla ya kwenda kufurahia mafanikio makubwa zaidi kule Barcelona.

Suarez alishinda mara mbili tuzo ya Kiatu cha Dhahabu wakati akicheza pale Camp Nou, akifunga mabao 195 na kutoa pasi za mwisho 112. Pia alishinda mara nne taji la LaLiga, taji la Copa Del Rey (Kombe la Mfalme) mara nne na mataji matatu msimu wa 2014-15, likiwamo la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #9. ROBERT LEWANDOWSKI

Nyota wa timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski, mmoja wa washambuliaji wamaliziaji bora zaidi kwenye historia ya mchezo huo. Amebarikiwa kwa kuwa na jicho la goli, amefunga mabao 454 katika klabu nne tofauti.

Lewandowski alianza maisha ya soka katika klabu ya nyumbani kwao Poland ya Znicz Pruszkow. Baada ya kucheza kwa muda Lech Poznan, alihamia kwa majirani zao Ujerumani ambako alijiunga na Borussia Dortmund.

Ilikuwa ni pale Dortmund ambako Lewandowski ndiko alijenga jina lake akifunga mabao 103 katika mechi 187 na kushinda mataji mawili ya Bundesliga na timu hiyo inayotumia jezi yenye rangi nyeusi na njano. Baada ya misimu minne, akaondoka hapo Dortmund na kwenda kwa wapinzani wao, Bayern Munich.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ameweka historia ya heshima yake hapo Munich - akishinda mataji nane mfululizo ya Bundesliga pamoja na Ligi ya Mabingwa na Klabu Bingwa Dunia pamoja na mchezaji bora wa msimu.

Lewandowski amefunga mabao 73 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumfanya kushika nafasi ya tatu kwa wafungaji wa wakati wote wa mashindano hayo.

### #8. FILIPPO INZAGHI

Huyu ni gwiji wa Juventus, AC Milan na Italia na bila shaka yoyote, Filippo Inzaghi alikuwa mchezaji bora zaidi kuvaa jezi namba tisa.

Inzaghi alifurahia mafanikio yake akiwa pale Rossoneri, ambako alishinda mara mbili Ligi ya Mabingwa Ulaya na mataji mawili ya Serie A, moja la Klabu Bingwa Dunia na Coppa Italia.

Anashika nafasi ya saba kwa wafungaji bora wa Italia na anashikilia rekodi ya kufunga 'hat-tricks' 10 kwenye Serie A. katika moja ya mafanikio yake, Inzaghi alifunga mabao mawili dhidi ya Liverpool kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2007 kuwasaidia Rossoneri hao kupata ushindi wa mabao 2-1.

Inzaghi alifunga mabao 25 katika mechi 57 na timu ya taifa. Alishinda Kombe la Dunia mwaka 2006.

### #7. MARCO VAN BASTEN

Marco Van Basten alikuwa mmoja wa mastraika bora zaidi miaka ya 80' na kuisaidia Uholanzi kushinda Kombe la Euro mwaka 1988.

Van Basten alikuwa mshambuliaji aliyekamilika zaidi na alifurahia mafanikio akiwa Ajax Amsterdam na AC Milan. Alishinda mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya msimu wa 1988-89 na 1989-90.

Akiwa AC Milan, alishinda tuzo ya Ballon D'Or mwaka 1988 na 1989 na kwa mara ya tatu mwaka 1992. Raia huyo wa Uholanzi wakati anastaafu soka pale Milan, alikuwa amefunga mabao 277 na kutoa pasi za mwisho 82 katika mechi 373.

### #6. GABRIEL BATISTUTA

Gwiji wa Fiorentina na Argentina, Gabriel Batistuta.

Batistuta alikuwa na misimu tisa ya kufurahia zaidi mafanikio pale Fiorentina akifunga zaidi ya mabao 200 katika mechi 331 na kuingia kwenye historia ya kipekee klabuni hapo.

Akiwa anajulikana kwa jina la 'Batigol', alimalizia soka lake pale AS Roma, akifunga mabao 184, anashika nafasi ya 11 kwa wachezaji waliofunga mabao mengi zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu Italia, Serie A.

Pia raia huyo wa Argentina, alishinda taji la Copa America 1991 na ndiye alikuwa anashikilia rekodi ya kuifungia mabao mengi timu ya taifa (56) iliyodumu kwa kipidi cha miaka 15, kabla ya kuvunjwa na Lionel Messi mwaka 2016.

### #5. ALAN SHEARER

Alan Shearer alikuwa mshambuliaji wa hatari zaidi katika zama za soka la kisasa.

Akiwa shabiki wa Newcastle tangu utotoni, Shearer akaitosa klabu hiyo na kwenda kusajiliwa Southampton wakati akiwa kinda. Akianza kuichezea akiwa na umri wa miaka 17, haraka Shearer akaingia kwenye vitabu vya historia wakati alipofunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Arsenal. Akasajiliwa Blackburn Rovers ambako alifunga mabao 112 kwenye Ligi Kuu katika mechi 138 alizocheza na kuiongoza Blackburn kushinda taji la EPL.

Halafu akaenda kujiunga na klabu yake kipenzi tangu utotoni, Newcastle United kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 15.

Shearer huko ndiko alikoweka rekodi ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Ligi Kuu England akifikisha mabao 260.

### #4. JOHAN CRUYFF

Awali alikuwa akivaa jezi namba 14, lakini Johan Cruyff baadaye akatambulika zaidi kwa jezi namba tisa mgongoni.

Alikuwa na mafanikio makubwa kwenye jezi namba tisa akiwa mchezaji na baadaye pia kupata mafanikio akiwa kocha.

Mholanzi huyu ndiye aliyebuni na kuanzisha akademi maarufu ya Barcelona ya kukuza vipaji vya soka kwa vijana 'La Masia', ambayo ndiyo iliyowatoa nyota wake wakali kama Lionel Messi, Andres Iniesta na Xavi.

Alishinda tuzo ya Ballon D'Or mara tatu na mwaka 1999, Cruyff alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa Karne wa Ulaya. Alifunga mabao 260 na pasi za mwisho 136 katika mechi 501 kwenye mashindano yote ngazi ya klabu.

### #3. GERD MULLER

Mmoja wa wafungaji bora kwenye historia ya mchezo huo, Gerd Muller - ambaye alifunga jumla ya mabao 721 katika mechi 769.

Mara zote alikuwa akijulikana kwa jina la utani la 'Der Bomber' (mlipuaji), Muller anachukuliwa kama mmaliziaji wa wakati wote, akifunga mabao 68 katika mechi 62 alizoichezea iliyokuwa Ujerumani Magharibi.

Alishinda Euro mwaka 1972 na Kombe la Dunia 1974.

Mchango wa Muller pia unatambulika sana pale Bayern Munich akiwa ameshinda mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na manne ya Bundesliga.

Mshindi huyo wa Ballon D'Or alitumia miaka 15 kuichezea Bayern Munich, akifunga mabao 523 na kutoa pasi za mwisho 101 katika mechi 580.

### #2. ALFREDO DI STEFANO

Alfredo Di Stefano alikuwa mmoja wa wachezaji bora walioubariki mchezo huo.

Raia huyo wa Argentina, ambaye baadaye akaamua kuchukua uraia wa Hispania, alikuwa nguzo muhimu kwa utawala wa Real Madrid na Hispania katika soka la dunia, karne iliyopita.

Di Stefano alishinda taji la Ulaya mara tano kuanzia miaka ya 50'. Alikuwa anavaa jenzi namba tisa na mshindi mara mbili wa Ballon D'Or.

Alfredo Di Stefano alikuwa mfungaji bora wa Real Madrid akitikisa nyavu mara 216 kabla ya kufunikwa na Raul mwaka 2009. Bado anashikilia rekodi pale Madrid ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa El Classicos (18).

Katika mechi 709 alizocheza ngazi ya klabu kwenye mashindano yote, alifuga mabao 519.

### #1. RONALDO NAZARIO

Huyu kwa waliomshuhudia hawana maneno mengi sana ya kumzungumzia zaidi ya kumtaja kama 'El Fenomeno', Ronaldo Nazario na bila shaka yoyote ndio mshambuliaji bora zaidi katika historia nzuri ya mchezo huo mzuri.

Wakati Cristiano Ronaldo amefuata nyayo zake kwenye kufunga mabao matamu, gwiji huyu wa Brazil anabaki kuwa ndiye Ronaldo kwa wale wote waliopata muda wa kutosha kumwangalia dimbani.

Alitumia muda wake wa kucheza katika nchi nne tofauti na mabara mawili, akipata mafanikio makubwa zaidi.

Mshindi mara mbili wa Ballon D'Or alichezea PSV Eindhoven katika misimu miwili, akifunga mabao 54 katika mechi 57.

Kwa ujumla amecheza mechi 119 katika klabu mbili pinzani nchini Italia, Inter Milan na AC Milan, akifunga jumla ya mabao 68. Alitumia msimu mmoja pale Barcelona na misimu mitano Real Madrid, akifunga jumla ya mabao 151 katika mechi 226 kwa timu hizo mbiliza Hispania.

Alirudi kwenye Ligi ya Brazil akifunga mabao 79 katika mechi 116. Pia akafunga mabao 62 na mechi 98 kwa timu ya Taifa ya Brazil.

Ronaldo Nazario ni mmoja kati ya wachezaji wanne walioshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Dunia mara tatu mfululizo. Ronaldo Luis Nazario de Lima ni mmoja wa wachezaji bora zaidi ambaye anaishi.


SUAREZ

## Nukuu

"Heshima zote kwa wachezaji niliofanya nao kazi... kwa kutazama kwa hivi karibuni, Manula [Aishi], Kapombe [Shomary], Luis [Miquissone] na Wawa [Pascal], wameonyesha uwezo mkubwa sana kwenye mashindano ya CAF, wanastahili kucheza klabu kubwa zaidi," **aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba (kwa sasa mshauri wa Yanga), Senzo Mbatha.**



"Barca hawakunithamini na Atletico wakanifungulia milango. Daima nitaishukuru klabu hiii kwa kuniamini," **Luis Suarez, baada ya kuipa Atletico ubingwa wa LaLiga juzi kwa kupiga bao la ushindi wakati wakiicha Real Valladolid mabao 2-1.**



"Licha ya matokeo, tunapaswa kujivunia kiwango cha kishujaa cha timu yetu. Wachezaji wetu walipambana kwa moyo na shauku kubwa hadi sekunde ya mwisho kabisa. Nitaendelea kusema kwamba tuna timu ya kushangaza. Ngoja tumalize ligi kwa nguvu. Tukutane mwakani #CAFCL!," **Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, baada ya timu hiyo kuichapa Kaizer Chiefs 3-0 na kutolewa kwa jumla ya mabao 4-3.**



# REKODI 5 KALI SIMBA IKITOLEWA CAF



Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akiifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA**

**Na Adam Fungamwango**

WANAUME wamefia vitani! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya wawakilishi wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, kutolewa kwenye michuano hiyo katika hatua ya robo fainali.

**Baada ya safari ya muda mrefu, hatimaye safari ya wawakilishi hao ilihitimishwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Simba ilihitimisha michuano hiyo kibabe kwa kuinyuka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Yalikuwa ni mabao mawili ya John Bocco na Clatous Chama yaliyoiwezesha timu hiyo kushinda, lakini bado ilikuwa inahitaji mabao mawili kuvuka au moja kwenda kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti.

Ni kwa sababu wiki moja iliyopita Simba ilifungwa mabao 4-0 nchini Afrika Kusini, hivyo mabingwa hao wa Tanzania kutolewa kwa jumla ya mabao 4-3. Licha ya kutolewa, Simba imeacha rekodi kadhaa ambazo zipo kwenye vitabu vya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), hizi hapa...

**#1. KWA MKAPA HATOKI MTU**

Wanachama na mashabiki wa Simba wana msemo wao kwa sasa 'Kwa Mkapa hatoki mtu'. Wakiwa na maana kuwa timu yao ikicheza uwanja wa nyumbani wa Benjamin Mkapa ni lazima washinde.

Na hilo limedhihirisha mpaka Simba inaondoka kwenye michuano hiyo, ikiwa imeshinda mechi zote za Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi na robo fainali, huku ikitoka sare moja na kushinda moja kwenye hatua za mwanzo.

Ilianza kwa kutoka sare nyumbani dhidi ya Plateua United ya Nigeria Desemba 5, mwaka jana, lakini kwa sababu ilikuwa imeshinda bao 1-0 ugenini ikasonga mbele.

Ilishinda mabao 4-0 dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe kwa Mkapa Januari 6, mwaka huu, baada ya kuchapwa 1-0 ugenini na baada ya hapo ikatinga hatua ya makundi.

Kwenye makundi ilishinda mechi zote tatu, bao 1-0 dhidi ya Al Ahly ya Misri Februari 23 na Machi 16 ikaitwanga Al Merrikh mabao 3-0, kabla ya kuishindilia AS Vita Club mabao 4-1, Aprili 3, mwaka huu na kisha hatua ya robo fainali ikaichapa Kaizer Chiefs 3-0.

Kwa maana hiyo Simba imecheza mechi sita kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu Uwanja wa Benjamin Mkapa bila kupoteza, ikishinda tano na kutoka sare moja tu.

**#2. KUONGOZA KUNDI**

Kwa mara ya kwanza kwenye historia ya soka la nchini, timu kutoka Tanzania imeongoza kwenye Kundi la Ligi ya Mabingwa Afrika. Simba iliongoza Kundi A, likiwa na bingwa mtetezi, Al Ahly ya Misri, baada ya kumaliza ikiwa kinara kwa pointi 13, ikicheza mechi sita, kushinda nne, sare moja na kupoteza moja.

Mbali na Al Ahly, pia kulikuwa na timu za AS Vita ya DR Congo, na Al-Merrikh ya Sudan.

**#3. ROBO FAINALI MARA NNE**

Simba imeweka rekodi ya kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara nne kwenye historia ya timu hiyo. Na ndiyo timu inayoongoza sasa kwa kufika mara nyingi zaidi kuliko timu yoyote nchini Tanzania.

Mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 1974. Ilitinga hatua hiyo kwa kuichapa Green Buffaloes ya Zambia mabao 2-1 nchini Zambia na Tanzania ikashinda tena bao 1-0, hivyo kutinga robo fainali kwa jumla ya mabao 3-1.

Na ndiyo mwaka ambao ilifanikiwa kwenda hadi hatua ya nusu fainali kwani baada ya hapo ilicheza mechi ya robo fainali dhidi ya Hearts of Oak ya Ghana, ikashinda ugenini mabao 2-1 na kupata suluhu nchini Tanzania, ikavuka hatua hiyo kwa mara ya kwanza, ambapo ilitolewa na Mehalla El Kubra ya Misri kwa penalti 3-0, kila timu ikishinda bao 1-0 nyumbani.

Kadhalika, mwaka 1994, ilifika robo fainali kwa kuifunga BTM Antananarivo ya Madagascar bao 1-0 nyumbani na ugenini ikatoka suluhu, lakini ikatolewa na Nkana Red Devils ya Zambia kwenye hatua hiyo kwa jumla ya mabao 4-3, ikichapwa 4-1 ugenini na kushinda mabao 2-0 nyumbani.

Mwaka 2019, ilitolewa hatua ya robo fainali na TP Mazembe ya DR Congo kwa jumla ya mabao 4-1, suluhu ya nyumbani na mabao hayo ikafungwa ugenini, kabla ya mwaka huu kutolewa tena kwenye hatua hiyo na Kaizer Chiefs.

**4. KUSHINDA UGENINI CONGO, NIGERIA**

Msimu huu Simba imeweka rekodi nyingine ya kuwa timu ya kwanza ya Tanzania kuzifunga timu kutoka DR Congo na Nigeria. Ilishinda ugenini bao 1-0 dhidi ya AS Vita Club Februari 12, mwaka huu, lakini pia ikashinda nchini Nigeria bao 1-0 dhidi ya Plateau United. Tangu uhuru hakuna timu ya Tanzania iliyowahi kupata ushindi wowote kwenye nchi hizo.

**#5. MISIMU MITATU ROBO MARA MBILI**

Tangu mwaka 2019, Simba imetinga hatua ya robo fainali mara tatu. 2020 ilitolewa hatua za awali na UD Songo ya Msumbiji. Hiyo ni baada ya kutinga robo fainali na kutolewa na TP Mazembe. Mwaka huu imerudia tena rekodi ya mwaka 2019.

**JE, WAJUA?**



KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, ameungana na kocha mwenzake kutoka Argentina, Helenio Herrera (mara nne) na Muuruguay Enrique Fernandez ( mara tatu), kuwa makocha pekee kutoka nje ya Ulaya ambao wametwaa ubingwa wa La Liga mara nyingi zaidi.



# Serikali yatakiwa kasi kuondoa vikwazo uwekezaji viwandani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kushughulikia kwa haraka vikwazo vinavyowakabili wawekezaji hususani wa viwanda ili kuleta tija.

Akichangia juzi hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/22, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema kumekuwapo na vikwazo kadhaa ambazo vimekuwa vikiwakwamisha wawekezaji hapa nchini.

Akitolea mfano wa kiwanda cha Dangote, Chikota alisema kampuni hiyo inakabiliwa na kero ya bei ya gesi asilia anayouziwa na Dangote.

"Pia kampuni hii inakabiliwa na changamoto ya meli baada ya kutaka kuanza kusafirisha saruji kutumia usafiri wa majini na pia Tume ya Madini imekipanga kiwanda hicho kama kampuni ya madini na kutaka kodi nyingi walipe," alisema.

Mbunge huyo alimshauri Waziri kuwa karibu na mwekezaji huyo kwa sababu kampuni yake imetoa ajira zaidi ya 500 kwa Watanzania, na ajira zisizo rasmi zaidi ya 2,000.

Kuhusu soko korosho, Chikota alipongeza serikali kwa hatua inazochukua kwa ajili ya soko hilo na kushauri yatafutwe masoko mengine mapya.

"Tusiende India kila mwaka, tutafute masoko mengine yapo mengi kama Vietnam, Japan na mengine mengi, naomba tutumie taasisi yetu ya TMX (Soko la Bidhaa nchini), kuhakikisha tunapata wanunuzi wapya wa korosho," alisema.

Mbunge huyo alisema kwa korosho inayotoka mipakani kama Msumbiji mara nyingine inaleta sintofahamu na kusababisha kuzuiliwa kuingizwa nchini.

"Naomba zile korosho za Msumbiji ziungane na kwetu ili kuongeza uzalishaji wetu, na wenzetu kule kwa yanayoendelea hawana soko, turuhusu ziingie bila kikwazo kwa kuwa wafanyabiashara wetu wanafanya biashara hiyo, kusiwe na vikwazo ambavyo sio vya lazima," alisema.

Aliomba serikali kutekeleza mradi wa Mchuchuma na Liganga kwa kuwa ni wa muda mrefu ni wakati sasa wa kuutekeleza.




Katibu wa Baraza la Utetezi la Watoto Wenye Ulemavu Wilaya ya Bahi, Yohana Msalali, anayesoma darasa la 7 Shule ya Msingi Bahi Sokoni, akizungumza na wazazi, walezi na watumishi wa serikali (hawapo pichani), kwenye mkutano wa uhamasishaji jamii kuhusu Elimu Jumuishi unaosimamiwa na Kanisa la Free Pentecostal Church Tanzania (FPCT) uliofanyika jana, wilayani Bahi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanaouza mazao nje wapewa somo kuepuka kudhulumiwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka wafanyabiashara wa mazao wanaosafirisha kwenda nje ya nchi, yakiwamo maharagwe ya soya, kujitambulisha kwenye balozi za Tanzania ili kuepuka kudhulumiwa au kupoteza fedha zao.

Bashe alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki katika kikao cha pamoja na wafanyabiashara wa zao hilo kuhusu mahitaji ya soko hilo nchi za nje.

"Tumepata haki ya kuuza soya katika soko la China, lakini haki hii ya kuuza soya hatuuzi peke yetu bali tunauza na wenzetu, ambao tunashindana nao katika biashara na miongoni mwa mataifa

ambayo tunashindana nayo ni Marekani, Brazil na mataifa ya Latin Amerika," alisema.

Bashe alisema mahitaji ya soya China ni metric tani milioni 115, lakini upungufu waliokuwa nayo ni metric tani milioni 87.

"Kuna mataifa ambayo yanazalisha sana soya na sote tunagombea soko hilo, kama Marekani wanazalisha wastani wa metric tani milioni 106 hadi 120, kitu ambacho kinatutofautisha sisi na wenzetu katika ushindani tulionao dhidi yao, ni kwamba tunauza soya ambayo ni non organic tofauti na wao," alisema Bashe.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa hiyo na kuwapongeza mabalozi wa Tanzania katika nchi za Malawi, Zambia na China kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa kuhakikisha wanapata na kufungua masoko ya bidhaa za Tanzania kwenye nchi hizo.

"Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki na timu yake walifanya kazi kubwa sana kwa ajili ya kufungua soko la China, na sasa hivi anapambana kwa ajili ya kufungua soko la tumbaku nchini humo na tayari Wizara imeshapeleka mfano wa bidhaa za tumbaku," alisema Bashe.

Aidha, alisema Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Benedict Mashiba na wa Zambia, Hassan Simba Yahya, nao wanapambana kutafuta masoko ya zao hilo na wamefikia hatua nzuri.

"Sasa wafanyabiashara mnapokwenda nchi za watu mjitambulishe katika balozi za Tanzania, ili kusaidia na kupewa mwongozo kwa mnachofanya."

"Hata mkienda katika nchi za Afrika ambazo zinatuzunguka hakikisheni mnafika katika balozi zenu, kwa sababu pale hudaiwi bali unakwenda kupata mwongozo na ulinzi kwa kitu unachotaka kwenda kufanya," alisema Bashe.

Aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa Wizara itashirikiana nao kuondoa vikwazo vyote, ambavyo wanakutana navyo katika kutafuta masoko ya biashara katika nchi mbalimbali.

# Mpango mkakati wa mahakama kwa miaka 5 waanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amezindua mpango mkakati mpya wa Mahakama ya Tanzania wa miaka mitano (2020/21-2024/25), ambao utatumika kama dira ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mahakama.

Prof. Juma alizindua mpango huo jijini hapa baada ya Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Mahakama nchini.

Alisema mpango huo ni muhimu kuutumia katika utendaji kazi wa kila siku kutokana na kwamba unaelekeza kila mtumishi anapaswa kufanya nini katika uwajibikaji.

"Nawapongeza sana watumishi wote kwa kazi mnazofanya, baada ya uzinduzi huu tukaendelee kuwajibika ipasavyo katika kazi zetu za kila siku," alisema Prof. Juma.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mathias Kabunduguru, alisema lengo la kuwa na mpango huo ni kuhakikisha kuwa Mahakama inafikia malengo iliyojiwekea katika suala zima la utoaji haki kwa wananchi.

"Huu ni mpango mkakati wa pili, ambao umelenga kuendeleza mazuri yote ya mpango wa kwanza, hivyo ni rai yangu kwa watumishi wa Mahakama na wadau washirikiane pamoja kama ilivyokuwa katika utekelezaji wa mpango wa awali ili kutekeleza ipasavyo azma yetu ya maboresho ya utoaji huduma bora kwa wananchi,"alisema.

Aidha, alisema kumekuwa na mafanikio katika utekelezaji wa mpango mkakati wa awamu ya kwanza wa mwaka 2015/2016-2020 na kuwapongeza watumishi kwa utekelezaji na kuwataka kuendeleza ari hiyo ya ufanyaji kazi kwa manufaa ya Mahakama na wananchi kwa ujumla.

Kabunduguru alisema katika mpango huo mpya utakuwa na nguzo kuu tatu kama ilivyokuwa katika mpango wa kwanza ambazo ni utawala, uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali, ili upatikanaji wa haki kwa wakati na kurejesha imani ya wananchi na ushirikishwaji wa wadau.

"Nguzo hizo zote zinaelekeza nini tunapaswa kufanya katika utendaji wetu wa kila siku," alisema.

Hata hivyo, aliongeza kuwa mpango mkakati huo una maeneo ya matokeo saba, malengo ya kimkakati 17 na viashiria vya matokeo 58.





## Polisi yakamata vinara tuhuma wizi wa pikipiki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu 163 kwa tuhuma mbalimbali wakiwamo vijana watatu ambao ni vinara wa wizi na uporaji wa pikipiki na kuziuza nchini Malawi.

Taarifa ya Jeshi la Polisi mkoani Mbeya iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana, iliwataja vijana hao kuwa ni Samwel Mwambenja (21), fundi magari, Brayton Nyangali (25) na Abdul Fumbo (24).

Taarifa hiyo ilieleza kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Mei 21, mwaka huu majira ya saa 7:30 mchana katika Kijiji cha Kasumulu, Kata ya Njisi wilayani Kyela.

Kamanda Matei alisema vijana hao huwa wanasafirisha pikipiki hizo kwenda nchini Malawi kwa Richard Ngoma, maarufu kwa jina la Pinda ambaye huwalipa ujira wa Sh. 120,000 kwa kila pikipiki.

"Pikipiki hizo huwa wanazivusha kupitia kwenye vipenyo visivyokuwa rasmi Mto Songwe, lakini mtakumbuka pia hivi karibuni tulimkamata mtu mmoja, Samwel Mwang'ombe (46), mkazi wa Uyole ambaye alikutwa na bajaji ya wizi yenye namba MC.321 CSA, ayoiiba hapa nchini na kwenda kuiuza nchini Malawi," alisema Kamanda Matei.

Katika tukio lingine Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali ambazo ni viazi pori maarufu kwa jina la 'Chikanda'.

Aliwataja watuhumiwa kuwa ni Moses Joseph (38), dereva wa gari aina ya Canter Custom yenye namba za usajili T.667 AJA na Hezron Kapokela (47), utingo wa gari hilo na mkazi wa Mbozi, mkoani Songwe.

Kamanda Matei alisema watu hao walikutwa na magunia 23 ya viazi hivyo na pia Jeshi hilo linawashikilia watu wengine 11 ambao walikuwa wanashirikiana na watu hao.

Vilevile, alisema watu wengine wanashikiliwa kwa makosa ya kukutwa na mali za wizi na wengine kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi bila kuwa na vibali.

Mkoa wa Mbeya umekuwa ukikabiliwa na matukio mbalimbali ya mauaji ya waendesha pikipiki na kutorokea kusikojulikana na pikipiki hizo.

# TANAPA kutumia vijana elimu ya uhifadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limebuni mbinu mpya ya kuwatumia vijana wanaotoka kwenye vijiji vinavyozunguka Hifadhi za Taifa, kutoa elimu ya uhifahi ili kuongeza ulinzi na kupunguza migogoro baina ya hifadhi na wananchi wa vijiji hivyo.

Mpango huo unaelezwa kuanza kwa majaribio katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Hifadhi ya Serengeti, ambazo zinakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ujangili. Mkuu wa Kitengo cha Ujirani mwema cha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Sharif Abdul, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wilayani Mbarali, wakati wa mafunzo kwa viongozi wa vijiji, kata na wilaya kuhusu mpango huo.

Alisema katika hifadhi ya Ruaha wana mpango wa kuufanyia majaribio katika vijiji 15 vya wilaya za Mbarali na Chunya, mkoani Mbeya, Iringa na Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, ambavyo vinapakana na hifadhi hiyo.

Alisema vijana hao watakuwa wanafanya kazi hiyo kwa kujitolea, lakini shirika hilo litakuwa linawapatia motisha ya fedha pamoja na vitu vingine yakiwamo mafunzo mbalimbali.

Alisema vijana hao watachaguliwa na wananchi wa vijiji husika na watakuwa wanawajibika kwa serikali ya vijiji kwa kutoa taarifa za utendaji kila mwezi.

"Vijana hawa ambao wanaitwa waelimisha jamii, watawajibika kufanya shughuli mbalimbali za kila siku za uhifadhi ikiwamo kutoa elimu kwa vikundi mbalimbali kama vyama vya akiba na mikopo (SACCOS), kwenye taasisi za dini pamoja na timu za mpira," alisema Abdul.

Alisema vijana watakaochaguliwa kufanya shughuli hizo wanatakiwa wawe na sifa mbalimbali ikiwamo elimu ya kidato cha nne, awe hana historia ya kufanya matukio yoyote ya uhalifu kwenye kijiji husika ikiwamo ujangili na kuwa na uwezo wa kuwasiliana vizuri kwa lugha ya Kiswahili pamoja na lugha za asili za maeneo husika. Akifungua mafunzo kwa viongozi hao wa serikali, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema mpango huo utakuwa na manufaa kwa wilaya hiyo ambayo ina vijiji vingi vinavyopakana na Hifadhi ya Ruaha na kumekuwa na uhusiano usiofaa baina ya wahifadhi na wanavijiji.

Alisema wananchi wamekuwa wakifanya mambo ambayo yanaingiliana na shughuli za uhifadhi kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu shughuli hizo za TANAPA na kwamba mpango huo unaenda kutatua tatizo hilo.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakifanya uharibifu hifadhini ikiwamo ujangili na uingizaji wa mifugo kwa sababu ya kuangalia maslahi yao binafsi badala ya kitaifa.

"Hawa waelimisha jamii watakuwa na uwezo wa kuhudhuria mikusanyiko mbalimbali ikiwamo mikutano ya vijiji, hivyo watasaidia kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ambayo yanawatatiza wananchi," alisema Mfune.

Baadhi ya viongozi wa serikali waliohudhuria mafunzo hayo, waliwashukuru maofisa wa TANAPA kwa kubuni mpango huo ambao walisema utasaidia kuimarisha ujirani mwema.

Diwani wa Kamata ya Miombweni, Jeremiah Kisagai, alisema kata yake ni miongoni mwa kata ambazo zimekuwa zikikabiliwa na migogoro ya mara kwa mara na maofisa wa TANAPA na mpango huo utasaidia kuimaliza.



Baadhi ya wavuvi wa samaki kwenye Mto Kiwira wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wakiwa wamepumzika wakisubiri mitego yao katika eneo la Chuo cha Magereza Kiwira juzi. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# 'Kila zahanati kuwa na nyumba 2 za watumishi'

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, inaandaa mapendekezo ya bajeti ili kuhakikisha kila zahanati inakuwa na nyumba mbili za watumishi wa afya.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali, Daniel Kamwela, wakati akizungumza na Nipashe mikakati ya kukabiliana na upungufu wa nyumba za wataalam wa afya.

Alisema, anatambua upungufu wa nyumba za wauguzi kwenye zahanati mbalimbali katika kukabiliana na kadhia hiyo, Ofisi ya Mkurugenzi itawasilisha pendekezo kwenye vikao vya mabaraza ya madiwani ili kujenga nyumba mbili za watumishi.

"Watumishi Sekta ya Afya wanafanya kazi nzuri licha ya kukabiliana na vikwazo mbalimbali, tumeandaa mapendekezo ya ujenzi wa nyunba mbili katika kila zahanati ili wauguzi wafanye kazi kwenye mazingira mazuri," alisema Kamwela.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Mbarali inakabiliwa na uhaba wa wauguzi na ili kukidhi mahitaji wanahitajika 402 na waliopo sasa ni 202 kutokana na ongezeko la kuanzishwa kwa zanahati na vituo vya afya.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema kuwa idadi ya wazazi wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma imeongezeka kutoka 13,740 kwa mwaka 2019 hadi 13,816 kwa mwaka 2020 na idadi ya vifo vya uzazi imepungua kutoka vinane kwa mwaka 2019 hadi vitano kwa mwaka 2020. Alisema idadi hiyo inatokana na jitihada za serikali kuboresha miundombinu kwenye Sekta ya Afya ikiwamo vifaa tiba, watumishi na majengo yanayojitosheleza. Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Mbarali, Eda Kidenya, alisema wauguzi wanaendelea kufanya kazi kwa juhudi pamoja na uchache walionao na kwamba wanaendelea kupata stahiki zao ikiwamo posho za sare za uuguzi kama mwongozo unavyotaka.



# Rai wadau kujipanga upya kuufufua utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani, amesema kwa kipindi cha mwaka mmoja, sekta ya utalii imeathirika sana kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19, na kuwataka wadau kujipanga upya.

Aliyasema hayo wakati akifungua tamasha la Kimataifa la Maonyesho ya Biashara ya Utalii Zanzibar mwaka 2021 (Zanzibar Holiday Market Festival 2021) Mjini Zanzibar.

Alisema maonesho hayo yana umuhimu wake ambayo yanahusiana na sekta ya utalii, ambayo imeathirika kwa ugonjwa huo, hivyo tamasha kama hilo linatoa matumaini ya kuanza upya huduma za utalii.

Alisema mataifa mengi hasa ya Ulaya wameanza kutoa chanjo kwa watu wao na wameanza kujiandaa kwa ajili ya safari, hivyo matamasha kama hayo ni muhimu katika kukaribisha msimu ujao wa utalii.

"Ni muhimu wadau wa utalii kukutana kabla ya msimu mpya wa utalii kuanza kujadiliana kwa kina ili kuboresha mazingira ya biashara," alisema.

Alisema kuwa tamasha hilo limefanyika wadau wengi wa utalii waliwa katika hali mbaya ya kiuchumi, kutokana na COVID-19, hivyo ni vyema kujipanga tena kulitangaza tamasha hilo nchi mbalimbali ili kuwafutia watu wengine zikiwamo nchi jirani.

Alisema fursa na uwezo wa tamasha hilo kuingia katika kalenda ya matukio ya kitalii Zanzibar ni kubwa sana, hivyo ni kujipanga na kushirikiana kuliendeleza tamasha hilo.

Naye Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatos Richard, alisema benki hiyo ni wadau wakubwa wa utalii na wamekuwa wakishirikiana na serikali na wadau wa utalii ili sekta hiyo ifanye vizuri. Alisema wanaisadia serikali kukusanya mapato pamoja na malipo yanayohusiana na utalii kwa njia za kidigital ili kurahisha malipo. "Zanzibar imekuja na kauli mbiu ya uchumi wa buluu, hivyo tunawasadia vijana katika utalii ili kuimarisha utalii wa Zanzibar," alisema.

Aidha, alisema wanatoa elimu kwa vijana kwenye masuala ya uchumi ikiwamo uvuvi na kilimo cha mwani, hivyo benki hiyo ni sehemu ya mkakakti wa serikali na wadau muhimu wa utalii ili sekta hiyo isonga mbele.

Ali Mtumwa Omar, ofisa masoko kutoka Kamisheni ya Utalii, alisema lengo la tamasha hilo ni kuwakutanisha wadau wa utalii, kutangaza fursa mbalimbali za sekta hiyo ili kuendeleza sekta ya utalii.

"Tunatangaza utalii na kwa sasa tupo katika uchumi wa buluu nguvu zetu tumeelekeza katika uchumi wa buluu kwa sababu utalii na uchumi wa buluu ni kama watoto pacha," alisema.

Alieleza kuwa wataendelea kuutangaza utalii ndani na nje kwa sababu lengo la Serikali ni kuongeza idadi ya watalii kutoka 530,000 hadi milioni moja, kama ugonjwa wa Corona duniani utapungua.

Tamasha hilo limeandaliwa na wadau wa Sekta ya utalii ikiwemo Jumuiya ya Watembeza Watalii Zanzibar (ZATO) na Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI).



Washiriki wa tamasha la kwanza la Jumuiya ya Watembeza Watalii Zanzibar (ZATO) linalofanyika mjini Zanzibar, wakimsikiliza Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko Zanzibar, Omar Said Shaaban (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa tamasha hilo jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Jamii yatakiwa kushirikiana na wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi Idara ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Juma Ali Simai, ameitaka jamii kutoa ushirikiano kwa idara hiyo, ili watu wenye ulemavu kupata haki sawa na wasio walemavu.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipofanya ziara kutembelea Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa akili iliyoko Dole Wilaya ya Magharib 'A' Unguja pamoja na kuwatembelea baadhi ya watoto wenye ulemavu wa aina tofauti katika vjiji vya Kama, Mtopepo na Meli nne Uzi.

Alisema si vyema kwa mtu mwenye akili timamu kuwakejeli, kuwabagua na kuwadhalilisha watu wenye Ulemavu kwa njia yeyote bali wanachotakiwa ni kuonyesha upendo kwa kuwapa malezi na matunzo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu mfuko wa uwezeshaji kwa watu wenye ulemavu kwa waombaji wa fedha za mfuko huo, aliwataka kuwa na subira kwa vile hivi sasa wanafanya uhakiki na mapitio ili kuwafahamu waliopewa fedha hizo na kuzirudisha kwa mujibu wa makubaliano ili malengo yake yaweze kufikiwa .

"Tumebaini kuna watu wamepewa fedha za mkopo, lakini hawana vigezo na sifa ... wapo waliopewa, lakini ukiwapigia simu wanasema hawajachukua mkopo, wengine tumebaini taratibu za malipo zimekiukwa wakati wa urejeshaji badala kulipa benki, hivyo kupelekea kasi ndogo ya urejeshaji wa fedha za mkopo," alisema.

Alisema kutokana na hali hio, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu inafanya mapitio ya muongozo wa mfuko uendane na hali halisi ya madhumuni ya mfuko wenyewe ili uweze kutoa huduma zaidi ya unavyotakiwa

Kwa upande wao watu wenye ulemavu kutoka maeneo tofauti waliotembelewa, waliomba kupatiwa dawa kwa wagonjwa wenye maradhi ya kuanguka, kusaidiwa vyerehani kwa vikundi vyao ili kujiendeleza kimaisha

# Othman ahimiza hadhari dhidi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, ameitaka jamii kufuata miongozo ya afya na kuongeza hamasa ya mapambano ili kujikinga ugonjwa wa Corona.

Makamu wa Kwanza aliyasema hayo Mjini Zanzibar katika hafla makabiadhiano ya vifaa vya kupima virusi vya corona.

Alisema ni jukumu la kila mtu kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo, ikiwamo kufuata maelekezo ya watalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinachukua jitihada kubwa ya kupambana na ugonjwa Corona, na kwamba vifaa hivyo vitasaidia kuongeza kasi ya kiwango cha upimaji wa virusi vya ugonjwa huo katika jamii.

Alieleza kuwa ugonjwa wa corona umeithiri sana dunia, hivyo ni vyema kushirikiana na wafadhili na wadau mbalimbali katika kujenga miundombinu mizuri ya afya ili kuepukana na maambukizi.

Othman aliwataka wafanyakazi wa Wizara ya Afya kuitumia vyema msaada huo kwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Akizungumzia hali ya maambukizi nchini, alisema ugonjwa upo, lakini hali sio mbaya, hivyo aliwasisitiza wananchi kuwa watulivu na kutosikiliza taarifa potofu zinazotolewa katika mitandao ya kijamii ili kuepuka taharuki.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema ugonjwa corona ni tishio duniani , hivyo ni vyema jamii kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya ili kujikinga na maambukizi.

Alieleza kuwa vifaa hivyo ni vyenye ubora wa hali ya juu, ambavyo hutoa majibu ya papo kwa papo na vitasaidia kugundua kwa haraka wale wenye kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Supplier CEO, Sunjay Patadia, alisema kampuni yake ina uwezo wa kutengeneza dawa na vitendakazi vyevye ubora kimataifa, na kwamba na vifa vipo tayari kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii bila madhara.

Vifaa hivyo vya haraka vya kupimia virusi vya Corona vyenye thamani ya Sh. milioni 250 vilitolewa na Kampuni ya SD BIOSENSOR na SUPLIER CEO kutoka ya Korea Kusini.

# Milioni 600/- zakusanywa vitambulisho ujasiriamali

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amesema serikali imekusanya Sh. milioni 600 zilizotokana na ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali.

Alisema hayo jana katika uzinduzi wa maonesho ya wajasiriamali yanayofanyika katika ofisi za kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi, kilichojumuisha taasisi za serikali na binafsi kilichopo Nyihogo, Manispaa ya Kahama.

Alisema kila mjasiriamali alilipia Sh. 20,000 kupata kitambulisho huku akitoa mfano kiasi hicho cha fedha kinatosha kujenga kituo cha afya kimoja na zahanati.

"Serikali inawajali wajasiriamali, lakini haiwezi pia kusaidia mtu mmoja mmoja ndio maana wanatakiwa wajiunge vikundi ili waweze kukopesheka, zamani mamalishe na baba lishe walikuwa wakidharauliwa, mtu kula kwao anaonekana ni wa hali ya chini, lakini hivi sasa wanaheshimika na wamepiga hatua," alisema Macha.

Alisema serikali ilikuwa ikipoteza mapato kwa kutotambua kundi hilo huku akiwaomba kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuzifunga vizuri ili ziuzwe katika maduka mbalimbali.

Mratibu wa Chuo Kikuu Huria, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Oscar Damasi, alisema kituo cha wajasiriamali kilianzishwa mwaka 2018 na kinajumuisha taasisi za serikali na binafsi.

Alisema lengo la kituo hicho ni kutimiza malengo mbalimbali ya wafanyabiashara wa sasa na wanaotarajia kuanza baadaye.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya maonesho hayo, Saimon Cheyo, alisema wajasiriamali 250 wanashiriki maonesho hayo.

Alisema kituo hicho kilianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi kiuchumi kwa kushirikiana na taasisi ya GSI Tanzania.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akiwasilisha taarifa yake wakati wa Mkutano Mkuu wa 26 wa Wanahisa wa benki hiyo uliofanyika mara ya kwanza kwa njia ya mseto, ambapo wengine walihudhuria katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC). Zaidi ya wanahisa 1,400 walishiriki Mkutano huo baada ya mafanikio ya Mkutano Mkuu wa 25 mwaka jana. Katika Mkutano huo, wanahisa waliidhinisha pendekezo la gawio la Shilingi 22 kwa hisa na hivyo kufanya jumla ya gawio la Sh. bilioni 58 kwa wanahisa wote. **NA MPIGAPICHA WETU**

# 400 washiriki maonyesho ya kilimo

**Na Christina Mwakangale**

WAKULIMA 450 wa zao la mtama kutoka wilaya za Kongwa, Mpwapwa, Chamwino mkoani Dodoma, wameshiriki maonyesho ya kilimo kuwajengea uwezo kukuza uzalishaji wa zao hilo.

Wakulima walijifunza mbinu mbalimbali za kuendesha kilimo cha kisasa na matumizi ya teknolojia itakayowawezesha kuongeza uzalishaji na kukutana na wadau muhimu katika sekta hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wa mtama, Leonard Yeramu, kutoka Kongwa, aliishukuru kuwawezesha kushiriki na wamejifunza mbinu mbalimbali kuhusiana na kilimo cha mtama.

Alisema moja kwa moja wakulima wamepata ujuzi, kushikamana na kuwawezeshwa kifedha na kuongeza uzalishaji wao.

Maonyesho hayo yalindaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushrikiano na Kampuni ya Bia Tanzana (TBL), yalifanyika mwishoni mwa wiki.

Wakulima hao ambao ni wadau muhimu wa kampuni ya TBL, huiuzia kampuni hiyo malighafi kwa asilimia 74 na tani 9,000 za mtama kwa ajili ya kutengeneza chapa maarufu za vinywaji vya bia aina ya Eagle na Bingwa.

Mwaka jana, TBL Plc kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Farm to Market Alliance (FtMA), iliendesha mradi wa majaribio kwa kuwawezesha wakulima 2,000 mkoani Dodoma kwa kuwapatia mbegu bora.

Wakulima walipatiwa huduma ya bima ya kilimo, itifaki za usimamizi wa mazao, ushauri wa kilimo kwa ajili ya kuhakikisha wanaongeza mavuno na soko la uhakika wa mavuno yao.

Kampuni hiyo pia ilishirikiana na TARI kufanya utafiti na kukuza mbegu za mtama ambazo zinafaa zaidi kwa ardhi na mazingira ya hali ya hewa ya Tanzania.Mradi huo ulifanikisha kuongeza uzalishaji wa zao la mtama kwa asilimia 70 na kufanya kazi na wakulima 4,000 katika msimu huu wa mwaka huu.

# Wanahisa Benki ya CRDB waongezewa gawio

**Na Christina Mwakangale**

WANAHISA wa Benki ya CRDB wameidhinisha gawio la Sh. 22 kwa hisa lililopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo.

Waliidhinisha katika mkutano mkuu wa 26 wa wanahisa uliofanyika kidijitali Mei 22, mwaka huu, jijini Arusha.

Gawio hilo ni ongezeko la asilimi 29.4 ya gawio lililoidhinishwa mwaka jana, linatokana na matokeo mazuri ya kifedha ya benki hiyo katika mwaka wa fedha 2020 baada ya kutangaza faida ya Sh. bilioni 165.2 licha ya matatizo ya ugonjwa wa COVID-19.

Akiwasilisha taarifa, Mwenyekiti wa hiyo, Dk. Ally Laay, alielezea kuwa utendaji endelevu na mabadiliko ya kimkakati yanayoendelea ndani ya benki hiyo yamesaidia kufungua uwezo wa benki, katika kuwahudumia wateja na kusaidia kuweka mazingira mazuri ya biashara.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, utendaji wa benki ya CRDB umeendelea kuimarika na kufanya uwekezaji wa wanahisa kuwa wa tija zaidi.

"Licha ya changamoto ambazo tulikutana nazo mwaka jana, tulijidhatiti katika kuhakikisha wanahisa wetu wanapata faida kutokana na uwekezaji wao kwa kila hisa. Tulipendekeza gawio la Sh. 22 kwa kila hisa na ninafurahi kuwajulisha kuwa wanahisa wamelidhinisha, "alisema Dk. Laay.

"Jumla ya gawio lililopendekezwa ni Sh. bilioni 58, ambalo linaashiria ukuaji wenye nguvu na maendeleo katika mapato kwa kila hisa na gawio kwa kila hisa.

Dk. Laay alibainisha, kipindi cha mwaka jana, benki ilipata mjumbe mpya wa bodi, Ellen Rwijage, ambaye alijiunga na kama mwakilishi wa Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA (DIF), ambao unamiliki hisa kwa asilimia 21 ndani ya benki hiyo.

Wakati huohuo wanahisa waliidhinisha mabadiliko ya katiba yaliyopendekezwa na bodi ya wakurugezi pia kupigakura kuchagua wajumbe wawili, Prof. Faustine Bee, ilichaguliwa kwa mara ya pili kuwakilisha wanahisa wenye umiliki chini ya asilimia moja na Gerald Kasatu alichaguliwa kuwakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja hadi 10.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alibainisha mapato ya benki na kampuni zake yaliongezeka sana licha ya kushuka kwa uchumi sababu ya janga la corona.

Alisema mapato ya uendeshaji yalisajili ukuaji wa asilimia 10.4 kufikia Sh. bilioni 854, ikilinganishwa na Sh. bilioni 774 zilizoripotiwa mwaka uliopita.

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa benki hiyo na Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, aliipongeza menejimenti na wafanyakazi kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo imeongeza ukuaji katika viashiria vyote muhimu vya utendaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020. Aliihakikishia bodi na menejimenti kuwa wanahisa wana imani nao na wataendelea kushirikiana nao kikamilifu.

# Ndalichako awaahidi neema wabunifu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itaboresha sera, miongozo na mazingira kwa ajili ya kuruhusu shughuli za kibunifu kufanyika katika mazingira ya kiushindani na kukua zaidi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifunga wiki ya ubunifu.

Alisema maboresho hayo yatalenga katika maeneo ya ushindani, ulinzi kwa wabunifu wenyewe, usajili, ulinzi katika kazi za wabunifu pamoja na masuala ya ujuzi.

Maeneo mengine ambayo alisema wanatarajia kufanyia maboresho ni katika kuhakikisha kwamba wabunifu wanapata kipato kupitia kazi zao za kibunifu hususani kwa kushirikisha sekta binafsi kuwekeza katika kukuza sekta hiyo na kuzitumia kwenye viwanda.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia sekta hiyo ya ubunifu kukua zaidi na kutumia teknolojia ya kidijitali katika soko la ushindani.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, Wizara yake imejipanga kuhakikisha kwamba masuala ya kidijitali yanaunganishwa kwenye mitaala katika viwango vyote vya elimu kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu.

"Hii itatusaidia kutoa wahitimu wenye uwezo wa kuajilika, wenye uwezo wa kushindana katika mabadiliko haya ya teknolojia ya kidijitali," alisema.

Alisema serikali imedhamiria kuendeleza bunifu kwa kuziorodhesha, kuzitambua na kusaidia wabunifu katika nyanja zote.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Christine Mususi, alisema wamezindua mpango mpya unaojulikana kama Fagio utakaoendelea katika kuendesha shughuli za ubunifu kwa kushirikiana katika kuwawezesha wabunifu kiuchumi.

Mpango huo mpya utafanyika kwa kushirikiana kati ya UNDP, Umoja wa Ulaya (EU), British High Commission, HDIF pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mkurugenzi Mkazi wa HDIF, Joseph Manirakiza, alisema bado kunahitajika nguvu ya pamoja kuendeleza shughuli za ubunifu nchini hususani katika eneo la uwezeshaji kiuchumi, kuwajengea uwezo wabunifu na kuboresha sera kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri kwa wabunifu ili wanufaike na kazi zao.

## RC mpya wa Lindi aja na mwarobaini wa umasikini

**Na, Said Hamdani,** LINDI

MKUU mpya wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Rajabu Tareck, ametaja njia zitakazosaidia wananchi kuondokana na umasikini unaowakabili.

Amezitaja ni kujenga mshikamano na ushirikiano katika kuzitumia fursa zilizopo, ikiwamo ardhi na madini kuimarisha maendeleo na uchumi wa Taifa.

Zainabu ametoa kauli hiyo wakati wa makabidhiano ya Ofisi kutoka kwa mtangulizi wake, Godfrey Zambi, yaliyofanyika mjini Lindi, na kuhudhuriwa na baadhi ya viongozi wakiwamo wa dini na vyama vya siasa.

Akipokea kijiti cha kuongoza Mkoa huo, Zainabu alishukuru mapokezi mazuri aliyoyapata kutoka kwa wananchi waliojitokeza, huku akiwaomba kumpatia ushirikiano aweze kutekeleza vyema majukumu aliyokabidhiwa na Rais wa Samia Suluu Hassan.

"Ndugu zangu wa Lindi, mimi ni binadamu, bila nyinyi sitakuwa na miujiza ya kila kitu nikifanye peke yangu, naomba mniunge mkono," Alisema Zainabu.

Zainabu ambaye alikwenda Shinyanga kukabidhi Ofisi, alisema ametoka mkoa wenye utajili mkubwa, yakiwamo madini, hivyo anapenda kuona Lindi inapaa juu kimaendeleo na kiuchumi kama maeneo mengine nchini.

Alisema Lindi ni miongoni mwa mikoa iliyo na utajiri mkubwa, ikiwamo ardhi ya kutosha, misitu iliyochanganyika na wanyama wengi, bahari na fukwe zake, gesi na madini, hivyo hakuna sababu kuendelea kuitwa masikini.

Alisema kuna umuhimu wa kuzitimia rasilimali hizo kutumika kwa kufanya mambo ya kimaendeleo ili kujikwamua kiuchumi.

Awali akitoa taarifa, Zambi alisema




Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru (watatu kushoto), akimkabidhi pikipiki Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Solelansabo, Mary James, wakati wa kongamano lilioandaliwa na Benki ya NBC lenye lengo la kuwapa mafunzo wanachama na viongozi wa vyama mbalimbali vya ushirika mkoani Tabora, yakiwemo umuhimu wa huduma za bima, matumizi ya fedha za kigeni pamoja na elimu ya kuweka kumbukumbu za hesabu na matumizi sahihi ya mapato yao ili waweze kukopesheka kwa urahisi wengine pichani ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo wa benki hiyo, Raymond Urassa (wa pili kushoto) na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika Mkoa wa Tabora, Absalom Cheliga (kushoto), pamoja na viongozi wa chama cha msingi Solelansabo, mkoani humo juzi. **NA PIGAPICHA WETU**

## Leseni zazuia uchimbaji holela dhahabu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

UTOAJI wa leseni kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu umesaidia kuzuia uchimbaji holela ambao unasababisha uharibifu wa mazingira.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Meneja wa machimbo ya dhahabu katika mgodi wa Kasi Mpya, eneo la Mwanzimba, wilayani Kahama, Cosmas Ndembuke, katika ziara ya waandishi wa habari kwenye mgodi huo.

Alisema kabla ya kupewa leseni na Wizara ya Madini, ulivamiwa na wachimbaji wadogo wakitafuta dhahabu kwa kubahatisha, huku wakiharibu mazingira kwa kuacha mashimo.

"Uharibifu wa mazingira kwenye migodi midogo, unatokana na uchimbaji wa madini kwa kubahatisha na ndiyo maana kuna mashimo mengi na mchimbaji asipopata dhahabu eneo hilo anahamia sehemu nyingine," alisema Ndembuke.

Naye Meneja programu na ufiti kutoka Taasisi ya kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini nchini (FADev), Evans Rubara, alisema ili kuzuia uharibifu huo wa mazingira migodini, inapaswa Wizara ya Madini iwe inatoa leseni kwenye maeneo ambayo yameshafanyiwa utafiti kuwa yapo badala ya kuchimba kwa kubahatisha na kuacha mashimo.

Ofisa kutoka ofisi ya madini ya wilayani Kahama, Marwa Geteny, ambaye anahusika na utoaji leseni, alisema mpaka sasa wameshatoa leseni 400 kwa wachimbaji wadogo.

# KOEMAN AJITETEA KUVURUNDA BARCELONA




**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anaamini msimu wake wa kwanza Barcelona unaweza kuchukuliwa kwa mtazamo chanya na anajiamini ataendelea kuwa kocha msimu ujao.

Barca iliifunga Eibar 1-0 kwenye mchezo wake wa mwisho wa LaLiga Jumamosi na kumaliza nafasi ya tatu, wakipitwa pointi tano na Real Madrid waliomaliza nafasi ya pili na pointi saba dhidi ya mabingwa wa LaLiga, Atletico Madrid.

Miamba hao wa Catalunya pia walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Paris Saint-Germain hatua ya 16-bora, na pia kufungwa na Athletic Bilbao Januari kwenye fainali ya Supercopa de Espana.

Kikosi cha Koeman kililipa kisasi na kuifunga Athletic kwenye fainali ya Copa del Rey mwezi uliopita na Koeman raia wa Uholanzi anahisi taji hilo limetosha kwa msimu huu.

"Tumeshinda pointi nyingi za ligi tangu kuanza kwa mwaka huu na tumeshinda kombe kwa kiwango cha kuvutia," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo wa mwisho pale Ipurua.

"Tulishinda kupaa kileleni wakati tulipokuwa na nafasi hiyo na tunatakiwa kujifunza katika hilo.

"Kama ungeniuliza Agosti kama tutashinda taji na kupambania LaLiga hadi mechi mbili au tatu za mwisho, ningekuwa na majibu tofauti.

# Ni hisia maalum kutwaa ubingwa LaLiga - Simeone

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesema mafanikio ya Atletico Madrid kutwaa taji la LaLiga msimu huu ni hisia maalumu hasa kutokana na mwaka kukumbwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Atletico iliifunga Real Valladolid mabao 2-1 pale katika dimba la Jose Zorrilla Jumamosi na kumaliza kileleni mwa msimamo kwa pointi mbili zaidi ya Real Madrid, ambao pia waliibuka na ushindi kama huo dhidi ya Villarreal juzi.

Hilo lilikuwa taji la 11 kwa Atletico na la pili kwa kipindi cha miaka tisa chini ya Simeone, akiwa pia ameshinda mara mbili Ligi ya Europa, UEFA Super mara mbili, Copa del Rey na Supercopa de Espana.

Na sasa Simeone anahisi kwamba, kikosi chake kilistahili kutwaa ubingwa huo licha ya mwaka kukabiliwa na mambo mengi magumu ndani ya uwanja na nje ya uwanja.

"Ulikuwa mwaka mgumu sana," alisema Simeone akiiambia Movistar+.

"Ni moja kati ya miaka bora zaidi kuwa bingwa. Nina furaha kubwa na watu wote wa hapa.

"Watu wengi wamepotea kutokana na virusi hivyo. Kwa Atletico kuwa mabingwa ni hisia tofauti kabisa."



# Lewandowski ajiwekea rekodi yake Bundesliga



**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski ameivunja rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao mengi zaidi kwa msimu mmoja wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, iliyodumu kwa miaka 49.

Awali Lewandowski aliifikia rekodi ya Muller ya kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja iliyowekwa msimu wa 1971-72 wakati Munich ikitoka sare ya 2-2 na Freiburg wiki iliyopita.

Na katika mechi ya mwisho ya msimu huu wa Bundesliga dhidi ya Augsburg, Lewandowski alifunga bao lake la 41 na hivyo kuingia kwenye kitabu cha rekodi mpya kabisa.

Katika mchezo huo, Munich walishinda mabao 5-2. Mara baada ya mchezo huo, Lewandowski aliiambia Sky Sport Ujerumani: "Sina maneno. Nilijaribu kufunga kwa dakika 90, nilijaribu kila kitu. Nina furaha kubwa sana."

Alipoulizwa endapo kuvunja rekodi hiyo ya gwiji Muller kama ni mafanikio makubwa zaidi katika kipindi chake cha uchezaji, Lewandowski alijibu: "Ulikuwa wakati wa aina yake na wa kihistoria".

# Zidane azungumzia hatima Real Madrid

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane atafanya mazungumzo na Real Madrid "ndani ya siku chache zijazo" baada ya timu yake kumaliza ikiwa haina taji lolote msimu huu.

Ushindi wa 2-1 dhidi ya Villarreal Jumamosi haukuwa mafanikio ya kujivunia, hasa baada ya wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid pia kushinda idadi hiyo ya mabao na kutwaa taji la LaLiga.

Mabao ya 'jioni' kutoka kwa Karim Benzema na Luka Modric yalionekana kuubadili mchezo huo kwa Madrid ambao walitanguliwa kufungwa kwa bao la Yeremy Pino na kuipa uongozi Villarreal.

Bao hilo lilimfanya Yeremy kuwa mchezaji kijana zaidi kufunga dhidi ya Madrid kwenye LaLiga katika karne ya 21, akiwa na umri wa miaka 18 na siku 214.

Villarreal wana fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Manchester United kule Gdansk, Poland Jumatano hii, lakini Madrid msimu wake umefikia mwisho.

Zidane anatarajiwa sana kuondoka, lakini alionyesha ishara ya kutulia baada ya mchezo huo dhidi ya Villarreal.

"Tunatakiwa kutulia. Nitazungumza na klabu kwa upole, lakini baadaye. Si sasa," alisema Zidane," akiwaambia waandishi wa habari.

"Ndani ya siku chache zijazo tutazungumza kuhusu hilo. Hivi karibuni tutaona nini kitatokea, si tu kuhusu mimi pia kwa klabu kwa ajili ya msimu ujao."



# PACQUIAO KUPANDA ULINGONI AGOSTI



**LOS ANGELES,** Marekani

BONDIA Manny Pacquiao amesema ana mpango wa kupanda ulingoni kuzipiga na bingwa wa mikanda ya EBF na WBC, Errol Spence Jr, uzito wa Welterweight Agosti 21, mwaka huu.

Pacquiao aliposti taarifa hiyo kwenye ukurasa wake wa Instagram mwishoni mwa wiki kuelezea pambano lake hilo ambalo litakuwa la uzito wa Welterweight.

Bondia huyo raia wa Ufilipino atarejea ulingoni kwa pambano lake la kwanza baada ya miaka miwili kuwa nje ya mchezo huo utakaopigwa Las Vegas nchini Marekani.

Kwa mujibu wa PBC na FOX PPV, Pacquiao mwenye umri wa miaka 42, alikuwa akitaka kurejea ulingoni kwa muda mrefu, lakini alikosa bondia wa kupigana naye.

Miezi michache iliyopita Pacquiao aliripotiwa kutaka kupanda ulingoni kuzipiga na Terence Crawford pambano ambalo lingefanyika Juni 5, mwaka huu kule Abu Dhabi, lakini ilishindikana.

Hata hivyo, kwa sasa bado hakuna taarifa rasmi kutoka kwa bondia Spence Jr kama yupo tayari kwa pambano hilo ama la.

# *Guardiola ataja miaka kwenda kuinoa Italia*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema akifikisha umri wa miaka 72 atakwenda Italia kuwa kocha na atamualika, Roberto Baggio kuwa msaidizi wake.

Baggio na Guardiola walicheza pamoja katika klabu ya Brescia, na bosi huyo wa City anaamini kuwa wanaweza kuwa pamoja sasa kama atakuwa kocha wa timu ya Taifa ya Italia.


Akizungumzia historia yake na Baggio, Guardiola alisema enzi zao alicheza nafasi yoyote na haikuwa rahisi kumshawishi nyota huyo wa zamani kuondoka Italia na Serie A.

Kwa mujibu wa Guardiola, wachezaji bora walipatikana Italia na kila mtu alipenda kucheza nchini humo.

Akizungumzia nia yake miaka ijayo alisema, anatarajia kwenda kuwa kocha pale atakapofikisha umri wa miaka 72.

"Nikiwa na miaka 72 na kuwa kocha wa Italia, nitamuomba (Baggio) kuwa msaidizi wangu," alisema Guardiola katika mahojiano na Sky Sport Italia.

"Nitajaribu kumrejesha kwenye ulimwengu wa soka. Lakini hauwezi kumshawishi Baggio, kwa sababu yeye ndiye mwenye maamuzi."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ: NIMELIPA DENI ATLETICO KWA UBINGWA

## ●●● Barca hawakunipa thamani yangu, lakini nikafungua milango hapa ili niweze...

**MADRID,** Hispania

AKITOKWA na machozi, Luis Suarez amesema mara zote ataikumbuka sana Atletico Madrid kwa kumpa nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kuondoka Barcelona.

**Suarez alikuwa nyota pale Barca tangu alipotua akitokea Liverpool mwaka 2014, lakini miaka yake sita ya kung'ara hapo Camp Nou ikaonekana si kitu wakati alipoambiwa hahitajiki tena klabuni hapo.**

Lionel Messi hakufurahishwa na uamuzi huo, na Barca imejikuta kwenye wakati mgumu msimu huu, huku Suarez akiwa shujaa kwa kuisaidia Atletico kubeba taji.

Atletico ilitwaa taji lake la 11 la LaLiga Jumamosi shukrani kwa bao la ushindi la Suarez na kuwafanya washinde 2-1 wakitokea nyuma dhidi ya Real Valladolid.

Hilo lilikuwa bao la 21 la Suarez kwenye LaLiga msimu huu akiwa amefunga mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye klabu ya Atletico.

Katika mahojiano na Movistar, Suarez akiwa anatokwa na machozi, alielezea jinsi alivyokuwa na deni hapo Atletico mara baada ya kumpa nafasi.

"Hali niliyopitia kipindi cha majira ya joto kilichopita ilikuwa ngumu sana, namna nilivyodharauliwa," alisema Suarez kweye umri wa miaka 34 raia wa Uruguay.

"Barca hawakunipa thamani yangu na Atletico wakafungua milango kwangu ili niweze kuendelea kuonyesha mimi ni mchezaji wa aina gani.

"Mara zote nitaikumbuka na kuiheshimu sana klabu hii kwa kuniamini mimi wakati ambao sikuaminiwa tena sehemu niliyoiamini."

## ZISIKUPITE

### ABRAHAM CHAMBO KWA RICE

CHELSEA wamefufua mpango wake wa kumuwania kiungo wa West Ham, Declan Rice na wanaweza kumtumia straika wake, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26, kuwa sehemu ya mabadilishano na nyota huyo. Manchester United na Manchester City pia zinamwania Rice, 22. ***(Sunday Telegraph)***

### CITY YAMFUNGUKIA KANE

MANCHESTER City ilitoa ofa kwa straika wa Tottenham na England, Harry Kane, 27, lakini ilikataliwa na Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ***(Sunday Mirror)***

### RASHFORD, SHAW KUUZWA

MANCHESTER United inaweza kuwatoa wachezaji, Marcus Rashford, Luke Shaw na Harry Maguire kwa ajili ya kumsajili Harry Kane katika Klabu hiyo. ***(Sun on Sunday)***

### KEITA KUTIMKA LIVERPOOL

KIUNGO wa Guinea, Naby Keita, 26, anataka kuondoka Liverpool na wakala wake amezungumza na Atletico Madrid juu ya uwezekano wa kujiunga na mabingwa hao wa LaLiga. ***(AS)***

### ROMERO AWANIWA JUVE

EVERTON na Juventus zinawania kumsajili golikipa wa Manchester United, Sergio Romero, 34, raia wa Argentina, ambaye anataka kuondoka Old Trafford baada ya kukosa namba msimu huu. ***(Mail on Sunday)***

### NUNO ATAFUTIWA MRITHI

KLABU ya Wolves inamfikiria kocha wa Porto, Vitor Pereira, 52, pamoja na yule wa zamani wa Benfica, Bruno Lage, 45, ili kuchukua nafasi ya Mreno mwenzao, Nuno Espirito Santo, ambaye anaondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu uu. ***(Mail on Sunday)***

### ZAHA ATAJA KLABU KUBWA

NYOTA wa Crystal Palace na Ivory Coast, 28, Wilfried Zaha, amesema kama "klabu Kubwa" zilitaka kumsajili yeye "hangekataa". Amekuwa akihuishwa na Arsenal na Everton. ***(The Face)***

### UNITED KUPELEKA OFA SPURS

MANCHESTER United ipo tayari kutoa ofa kubwa kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Tottenhapa Hotspur, Harry Kane, 27. ***(Sunday Times)***

### FLETCHER KUJIUNGA WATFORD

NYOTA wa Middlesbrough, Ashley Fletcher, 25, amekubali kujiunga na Watford kwa mkataba wa miaka mitano, mara tu atakapokuwa mchezaji huru mwezi ujao. ***(Sun on Sunday)***

### LEICESTER YAMWANIA RYAN

LEICESTER City ni klabu ya hivi karibuni kujiunga kwenye mbio za kumuwania mlinzi wa Southampton na England, Ryan Bertrand, 31, huku Arsenal na AC Milan pia zikimwania  ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Talksport)***

## Stars ya Ufukweni, Uganda vitani leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Tanzania cha Soka la Ufukweni (Beach Soccer), leo kitashuka dimbani nchini Senegal kuvaana na Uganda katika kibarua chake cha kwanza kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (BSAFCON) 2021, yaliyoanza kutimua vumbi jana.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawassa, alisema wamewasili nchini Senegal na kikosi kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya Uganda.

Alisema wamejiandaa vizuri na wamepata nafasi ya kuwasoma wapinzani wao Uganda katika mechi ya kwanza waliyocheza na Senegal jana kwenye mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo.

"Tumepata nafasi ya kuwaona wapinzani wetu, tumepata tathimini ya jinsi wanavyocheza, naamini ni tathmini nzuri kwa mechi yetu katika kuhakikisha tunaenda kufanya vizuri katika mechi yetu ya kwanza," alisema Pawassa.

Tanzania imepangwa Kundi A ya michuano hiyo pamoja na Uganda na wenyeji wa mashindano hayo, Senegal ambao wataikaribisha Tanzania Mei 26, mwaka huu.

## JKU hesabu sasa kwa Black Sailor

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kushushiwa kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya timu ya Polisi, JKU FC imesema itajipanga kuhakikisha Jumatano inafanya vizuri katika mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Black Sailor.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mau A jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Msellem Said, alisema kwa sasa hahesabu mchezo aliopoteza na baada yake anajikita kurekebisha makosa ili mechi ijayo aweze kupata alama tatu na kuinusuru timu hiyo kushuka daraja.

Alisema tatizo alililiona ni kwamba timu yake bado inarejea makosa yale yale ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi, lakini inashindwa kuzitumia kupata mabao.

"Tunaendelea kujipanga kufanya vizuri katika michezo yetu iliyobaki, tutarekebisha makosa ambayo tumeyaona katika mchezo huu ili timu iweze kupata alama tatu mchezo ujao," alisema.

# SIMBA IMELINDA HESHIMA MICHUANO CAF - MAKALLA

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewapongeza wachezaji wa timu ya Simba kwa kupambana na kulinda heshima ya Mkoa wa Dar es Salaam na nchi kwa ujumla kutokana na kutolewa kishujaa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Simba ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Makalla, ambaye aliteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu, alisema wachezaji wa Simba walipambana hadi mwisho na licha ya kushindwa kufuzu, wameweka heshima kubwa kwa nchi kwani isingekuwa vema kufungwa nyumbani.

**"Wameutumia vizuri uwanja wa nyumbani. Walifungwa 4-0 na wao wameshinda mabao 3-0. Wametolewa, lakini mwisho wa yote wametuwakilisha vizuri kwa sababu siku zote mshindi lazima apatikane. Niseme tu mpira umeisha. Simba wamepambana ndani ya nchi. Wamelinda heshima ya nchi. Yaani watupige kwao na hapa napo waje watupige? Haiwezekani kwa kweli. Tunawapongeza," alisema Makalla.**

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes da Rosa naye pia aliwasifu wachezaji wake akisema wamepambana hadi mwisho licha ya kushindwa kutumia baadhi ya nafasi zilizopatikana kufunga.

"Tumeondolewa, lakini imechangiwa kwa kiasi kikubwa zaidi kwa kuruhusu mabao kwa urahisi katika mchezo wa kwanza," alisema kocha huyo.

Jana baada ya mechi hiyo, baadhi ya viongozi, wanasiasa, wabunge, viongozi wa klabu mbalimbali, wanamuziki, na wasanii bila kujali timu zao, walipongeza Simba kwa mchezo safi waliouonyesha kwenye mechi hiyo hadi kupata ushindi wa mabao 3-0, ingawa haukuwawezesha kusonga mbele kwenye hatua ya nusu fainali kutokana na kufungwa mabao 4-0 nchini Afrika Kusini wiki moja iliyopita.




Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga (wa pili kushoto) na Msanii wa Bongo fleva kutoka Lebo ya WCB, Zuhura Othman Soud 'Zuchu', wakionyesha mkataba wa makubaliano ambapo msanii huyo atakuwa balozi wa mtandao wa Zantel 4G. Kushoto ni Mkuu wa Zantel-Zanzibar, Mohamed Khamis Mussa, pamoja na menejimenti ya Kundi la Wasafi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Zuchu atangazwa balozi wa Zantel 4G*

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Zantel imeingia makubaliano na msanii wa muziki kutoka Kundi la Wasafi 'WCB', Zuhura Othman Soud maarufu kama 'Zuchu', kuwa balozi wa mtandao wa Zantel 4G.

Tukio la utiaji saini makubaliano hayo lilifanyika jana katika makao makuu ya Zantel yaliyopo eneo Amani - Zanzibar na kushuhudiwa na menejimenti ya Wasafi pamoja na waandishi wa habari.

Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga, alisema kampuni hiyo ina imani kubwa na msanii huyo kutokana na ukweli kuwa ni moja ya kipaji kutoka Zanzibar na anaufahamu vema mtandao wa Zantel.

"Zantel kwa sasa tunaendesha kampeni yetu inayojulikana kama 'Pasua Anga Ki Zantel 4G' ambayo inalenga kufanya uelimishaji juu ya matumizi yenye tija ya mtandao wa 4G. Zuchu amekuwa mfano mzuri wa namna anavyotumia mtandao wa 4G kuendeleza kipaji chake na ameweza 'Kupasua Anga Kitaifa na Kimataifa," alisema Muga.

Aliongeza kuwa, mbali na uelimishaji, kampeni hiyo imelenga kuinua na kutambua vipaji kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo za michezo, muziki pamoja na uchekeshaji 'comedy'.

"Sote ni mashahidi juu ya namna gani msanii huyu alivyoweza 'Kupasua Anga' na kuwa mmoja wa wasanii wa kike mashuhuri hapa nchini. Zuchu anakwenda kuwa balozi wa kampeni yetu hii ya 'Pasua Anga Ki-Zantel 4G' ambayo itafanyika kwa muda wa miezi sita mfululizo," alisema.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Zuchu alisema: "Nimefurahi sana kuwa balozi wa kampeni hii ya Pasua Anga Ki Zantel 4G, ukizingatia mimi ni moja ya wasanii kutokea Zanzibar, hivyo naifahamu vizuri Zantel," alisema na kuongeza

"Intaneti ni kitu muhimu sana kwangu, siwezi kukaa saa 24 bila kuwa na mtandao hasa mtandao wa 4G ambao utaniwezesha kufanya mambo mbalimbali kwa haraka zaidi," alisema Zuchu.

Michezo
Jumatatu Mei 24, 2021
Nipashe



Suarez: Nimelipa deni Atletico kwa ubingwa UKURASA 22

CHA KWANZA...



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akifunga bao la kwanza kati ya mawili aliyoifungia timu yake wakati ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, kwenye mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Senzo awapaisha Manula, Miquissone

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANGO kilichoonyeshwa na wachezaji wa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kimemuamsha aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu (CEO) wa klabu hiyo, Senzo Mbatha na kuwataja baadhi kuwa wanastahili kucheza klabu kubwa zaidi.



Senzo, ambaye kwa sasa ni Mshauri wa uendeshaji wa klabu ya Yanga, ametoa heshima zote kwa wachezaji aliofanya nao kazi wakati akiwa Simba kutokana na ubora wao katika michuano hiyo ya CAF.

"Heshima zote kwa wachezaji niliofanya nao kazi... kwa kutazama kwa hivi karibuni, Manula [Aishi], Kapombe [Shomary], Luis [Miquissone] na Wawa [Pascal], wameonyesha uwezo mkubwa sana kwenye mashindano ya CAF, wanastahili kucheza klabu kubwa zaidi," aliandika Senzo kupitia mtandao wa Twitter.

Wachezaji hao walikuwa sehemu ya kikosi cha Simba kilichoibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Saam, dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, kwenye mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini timu yao ilitolewa kwa jumla ya mabao 4-3 kutokana na mchezo wa awali kupoteza 4-0 ugenini.

# Nurkovic aipigia saluti Simba

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Aitabiria makubwa, Gomes asifu wachezaji akililia bahati, Bocco ajazwa mamilioni...

STRAIKA hatari wa Kaizer Chiefs, Samir Nurkovic, amesema Simba ina timu nzuri sana na inaweza kufika mbali kama itapata tena nafasi ya kushiriki michuano hiyo mwakani, wakifanya marekebisho madogo tu.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi baada ya timu yake kufuzu hatua ya nusu fainali licha ya kuchapwa mabao 3-0, mchezaji huyo raia wa Serbia ambaye alifunga mabao mawili kwenye mechi ya kwanza wiki moja iliyopita nchini Afrika Kusini wakati wakishinda 4-0, alisema anashukuru kwa timu yake kufuzu, lakini wamepata ushindi huo kwa timu ngumu ya Simba ambayo iliwaelemea muda mwingi wa mchezo kwenye mechi hiyo ya marudiano, huku ikikosa nafasi nyingi za kufunga.

Alisema Simba ingeweza kuwatoa kwenye mashindano hayo kama wasingepata ushindi mkubwa kwenye mechi ya kwanza nyumbani katika Uwanja wa FNB.

"Tulitarajia mchezo mgumu, lakini kitu cha muhimu ni kwamba tumefuzu, tulishinda mchezo wa kwanza kwa kulazimisha, lakini wote tulijua Simba itacheza kwa kushambulia, lakini tumevuka," alisema Nurkovic na kuongeza.

**"Bila shaka, mara zote tunachukua mechi moja baada ya nyingine, na kuona kwa namna gani tutafika mbali, Simba ni timu nzuri sana na tulikuwa tunatarajia watakuja kwetu kwa presha kubwa, na kulazimisha sana kwetu, palikuwa hakuna cha kufanya zaidi ya kuzuia."**

Nurkovic alisema, Simba walikuwa wapinzani waliostahili kwao, lakini ushindi wao katika mechi ya kwanza ndio ulioleta tofauti.

"Kwetu, ilikuwa muhimu sana kwamba tulitengeneza nafasi nyingi katika mechi ya kwanza nyumbani na tulizitumia na sasa tumeshinda kwa tofauti ya bao moja limetupeleka nusu fainali."

Akiwazungumzia wapinzani wao, Simba, alisema ni timu nzuri sana na hawezi kukaa na kuwataja mchezaji mmoja mmoja, Nurkovic alisema yeye anaona kikosi chote ni kizuri na kinacheza kwa ushirikiano na kwa maelewano.

"Sijui sana habari ya ligi ya Tanzania, lakini naifahamu Simba kuwa ni timu nzuri na bora kabisa, yenye wachezaji wazuri, wanaocheza kwa ushirikiano na kwa maelewano. Kama wataendelea kukaa pamoja na kurekebisha vitu vichache msimu ujao wanaweza kufika mbali zaidi," alisema.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, akizungumzia mechi hiyo, alisema wamesikitika kutolewa katika mashindano kwa sababu walistahili kushinda ila haikuwa bahati kwao kusonga mbele.

"Licha ya kutolewa, nina kila sababu ya kujivunia kuwa kocha wa Simba na aina ya wachezaji wangu kupambana hadi hatua ya mwisho, walijitolea sana na wamepigana vizuri sana yaliyotokea ni katika mpira.

"Ni kweli tulipoteza nafasi nyingi dakika 45 za kwanza ila sina shida na washambuliaji wangu, nina wafungaji wanaofanya vizuri sina hofu nao wakati mwingine huwa ni habati, kwa hii haikuwa kwetu," alisema Gomes.

Katika mchezo huo mabao ya Simba yalifungwa na John Bocco ambaye klabu yake ilimtangaza kuwa mchezaji bora wa mechi na kuzawadi Sh. milioni 2.5, huku la tatu likifungwa na Clatous Chama.

Kaize Chiefs sasa hatua ya nusu fainali itacheza na Wydad Casablanca ambayo juzi iliichapa MC Alger bao 1-0 nyumbani, hivyo kusonga mbele kwa jumla ya mabao 2-1, kufuatia sare ya bao 1-1 ugenini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >